


NYUMBA YAKO

 . . . nawaambia, ingeninii—i . . . najua hamji huko kunisia mimi, mnaona, kwa sababu hakuna mtu angeendesha gari umbali huo kumsikia mhubiri. Mnakuja huko kwa sababu kwamba m—mnaamini Ujumbe na mnamwamini Kristo, nami ninathamini hilo.

² Nami ninashukuru sana kuwa na marafiki kama hao, kuwa na mtu ambaye—ambaye anathamini jitihada za—zako, hilo ndilo mnalajaribu kufanya, ku—kuendesha umbali huo juu ya hali hizo. Jambo pekee ninaloweza kusema, laiti . . . Nilimwambia Meda, nikasema, “Sijui kama tungeweza kuwaleta watu wote wanaotoka zaidi ya maili hamsini, huko juu nyumbani, kwa ajili ya chakula cha kutwa?” Mnaona? Sijui tungefanya nini nao, mnaona, kwa sababu sehemu kubwa zaidi ya kanisa letu, nadhani, asilimia themanini yao ni ninyi watu, mnaotoka Mississippi, Alabama, na Georgia, na mahali kama hapo, mnakotoka. Nanyi mnafikiri . . .

³ Na hakuna watu wanaokuja ambao ni matajiri, ni watu wa kawaida tu. Nami najua hilo linahitaji kuweka pesa zenu nyingi sana akiba kufanya hivyo, kwa sababu ninajua ni kiasi gani cha petroli kinachotumika kuja na kurudi, na mbali na hayo uchakavu wa gari, kwa kuwa safari ya kwenda na kurudi inakaribia, loo, nakisia ni kama maili elfu moja mia sita, mia saba kwa somo moja, na mnakuja hizo kila juma. Wazieni jambo hilo. Mnaona? Ninaninii tu, ninajisikia mdogo *hivyo*, kwa kweli, kama tu kwamba nilikuwa na urefu wa nusu inchi kusimama mbele zenu kuwaambia kweli jinsi mimi—jinsi ninavyolithamini hilo.

⁴ Mimi na mke wangu tulikuwa tukizungumza, kama ninyi watu hamkuja wakati ninapofanya ibada, maskani haingenilipia kwenda, maana kuna wengi katika chumba hiki, sasa hivi, kuliko wangukwako kama haikuwa ni kwa ajili yenu ninyi watu, hiyo ni kweli kabisa.

⁵ Na hilo linatimiza yale Maandiko yasemayo, “Katika nchi yetu wenyewe, miongoni mwa watu wetu wenyewe.” Wewe . . . He—heshima zako na taadhima yako daima hutoka kwa mtu wa nje, sijui ni kwa nini, lakini, simaanishi wa nje— . . . namaanisha kutoka nje ya nyumba yako mwenyewe. Bila shaka, nisingeweza kuwawazia ninyi nyote kuwa watu wa nje, ninyi ni ndugu wenzangu na raia katika Ufalme wa Mungu.

⁶ Na hapa siku moja, nilikuwa na maskini mamba mdogo wa bandia ameshindiliwa, hapa chini, nami nikamwambia Ndugu Welch nilikuwa nikishuka kuja kumchukua. Nao watoto hawakuweza kumaliza likizo yao, nami nikawazia

ningewapeleka Florida mbio, huko St. Petersburg asubuhi, tushuke twende, ninataka kupanda kwenda Miami na kuja huku kupitia Mkondo wa Tamiami, kisha nirudi nyumbani. Nao inawabidi kwenda shuleni mara moja, nami nilifikiri huu ungekuwa ni wakati mzuri wa kusimama huku kwa ajili ya huyo mamba.

⁷ Na kwa hiyo Ndugu Welch, uh, Ndugu Fred na Ndugu Wood walikuja pamoja nami, kwa hiyo hilo lingenipa nafasi ya kuwaleta hao watoto, nao watarudi na mamba wangu. Nami nikawazia, nilipokuwa hapa chini, ningetaka tu kuwa na... kundi lenu dogo pamoja, kuwaambia jinsi ninavyowathamini, jinsi ninavyothamani jitihada zenu.

⁸ Na Ndugu na Dada Evans, na—na Ndugu na Dada... Na—nalipata, naliita S. T., ninajua ya kwamba ni T. S. I... Kuna ki—kigogomozi, kisuuza kinywa wanachokiita S.T.37, na hivyo ndivyo ninavyowaita ninyi S. T. Sio kutoka... Na ni—ni kitu kizuri, pia, ni kizuri sana, kimevishinda hivyo vingine vyote, nionavyo mimi. Wanakitumia jeshini, nami ninakitumia kwa karibu chochote: kugogomolea, na kama kisuuza kinywa, na kukibeba nikienda mawindoni, ambapo farasi wangu akiumia, ninammwagilia hicho kidogo, mwajua, cho—chochote tu, ni—ni kizuri kwa kila kitu.

Nadhani, mnakipata hivyo pia, sivyo, Dada? Huko kote, kuosha vyombo wakati mwingine na kadhalika.

⁹ Na kwa hiyo, nilifikiri labda ningeliza usiku wa leo, nilimwambia Ndugu Welch, “Ungefanya nini...? Tunge sema nini jamaa wakija huku? Mnafikiri...?” Tulifikiri labda kama ulikuwa na swali dogo niani mwako, jambo dogo tu ambalo ungeweza, labda jambo fulani ambalo ningeweza kujibu, jambo fulani ambalo hungetaka kuchukua, labda, wakati wao huko maskanini wakati mkiwa huko, swali dogo, na hiyo ndiyo sababu nilipitia hapa.

¹⁰ Kwa hiyo, tunajua ya kwamba mnaenda kazini asubuhi. Ni saa tatu na dakika kumi, kwa hiyo tutaliingilia moja kwa moja. Lakini kabla hatujafanya hivyo, twaweza tu kuinamisha vichwa vyetu kwa maombi?

¹¹ Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha sana kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu, Yule—Yule aliyeziokoa nafsi zetu kutoka kwenye maisha ya dhambi, na ametufanya raia wa Ufalme Wake, kwa neema Yake tumeokoka, na huko, si sisi wenyewe, wala kwa matendo yetu, bali kwa rehema Zake tumeokoka, kwa hiyo tunafurahia jambo hilo sana. Nasi tunajua ya kwamba siku moja tutamwona, kwa kuwa tutakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe uliotukuka, nasi tutamwona jinsi alivyo. Kwenye wakati huu, bado hatujui jinsi hilo litakavyotukia, lakini si juu yetu kujua, tunalitazamia tu kwa imani, na mwenendo wote ni imani. Kwa hiyo, tunashukuru kwa ajili ya mambo haya.

¹² Tunaomba ya kwamba utawabariki watu hawa, Bwana. Nilipokuwa nikiendesha gari kuja hapa chini, Wewe unajua kilichokuwa mioyoni mwetu jana usiku, mimi na mke wangu, tulipokuwa tukizungumza barabarani. Jinsi, ambavyo, tunajisikia kuwa na furaha, kuwa na marafiki ambao wangejitolea kuja kuisikia Injili tukufu ya Mwana wa Mungu, wangeendesha gari mamia hayo yote ya maili mchana na usiku, wapate tu kusikia ujumbe mmoja.

¹³ Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utawapa, kila mmoja, makao matukufu katika ule Ufalme. Wabariki wanapokuwa hapa duniani, wafanikishe katika lolote wafanyalo, jalia lifanikiwe.

¹⁴ Na hawa watoto wadogo, Bwana, ni jamaa wadogo tu bado, na wengi wao hapa katika utineja, na hata hivyo wanaketi kwa uchaji na heshima kama mtu mzima, Mungu, nafikiri wao ndio walio bora sana nchini, ninaomba ya kwamba utawabariki, Bwana, jalia kamwe wasipungukiwe na chochote, na jalia, katika ule Ufalme mkuu huko ng'ambo, wakati familia yote itakapokusanyika pamoja, nina hakika watakuwa huko, Baba. Na—naomba ya kwamba utakuwa na kila mmoja wao huko, jalia wasigeuke kamwe kutoka kwenye njia hiyo nzuri iliyosonga, waliyofundishwa kupitia. Tujalie, Bwana.

¹⁵ Sasa usiku wa leo, niliwazia, Baba, tungetafuta kujua kilicho mioyoni mwa hawa watu. Unaijua mioyo yao, nami ninakuomba Wewe, Baba, ya kwamba utanisaidia kujibu maswali yao, ili yawe mema kwetu, kwamba ingekuwa vema kwetu kuwa hapa, nasi tungeweza kwenda mbele tukisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, kwa sababu ya Uwepo Wake?”

¹⁶ Njoo sasa, Bwana, tembea kwenye hivi viti, weka mkono Wako juu ya kila bega, usugue mkono Wako wenye kovu la msumari kwenye kila moyo, tupate kujua ya kwamba ni Bwana wetu aliye karibu, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁷ Nafikiri tuna Bi—Biblia hapa, ningetaka tu kusoma A—Andiko Hapa ndani, kwa dakika moja tu, tupate mwanzo mdogo, kabla hatujaingia kwenye somo, ama, maswali, hasa.

¹⁸ Na hili, ningetaka kusoma hili, ma—mahali nilipopata alasiri ya leo. Nilikuwa nikipanda juu, tukiendesha mimi pamoja na Ndugu Welch, kwenye kiti cha mbele cha gari la Ndugu Sothmann pale, nami nikasoma jambo fulani, nilifikiri ningetaka tu kulizungumzia, kwa dakika chache tu, kama ninaweza kulipata katika ninii yake . . . loo, naam, tumelipata.

¹⁹ Katika mlango wa 16 wa Matendo, na kuanzia yapata kifungu cha 37.

Paulo akawaambia, Wametupiga mbele ya watu wote . . .

²⁰ Samahani, hapo sipo ninapotaka hasa, mahali hasa nilipotaka kuanzia kusoma. Ni . . . Nilikuwa nikisoma mahali fulani humu ndani, ninii tu . . . Nitapapata hivi punde. Nimepapata, ni kifungu cha 29, kifungu cha 28, hebu tuanze.

Ila Paulo akapaza sauti yake kwa nguvu, akisema, Usijidhuru, kwa maana sisi sote tupo hapa.

Wakataka taa ziletwe, . . . akarukia ndani, akitetemeka, akaanguka mbele ya Paulo na Sila,

Kisha akawaleta nje, akasema, Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?

Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.

²¹ Ni mojawapo tu ya maswali haya madogo ya kupinda ambayo nilifikiri ningetaka kuyazungumzia kwa dakika moja tu, kuhusu *Nyumba Yako*, kwa kuwa ninawaona, kila mmoja, ni viziri sana kuweka nyumba yako katika utaratibu, wa—watoto wako wameokoka, na—na hilo—hilo ni jambo zuri kuifanya familia yako wawe wote Wakristo, kwa sababu mimi . . . tu—tunataka familia zetu, sisi, kila mmoja, tuwafikirie watoto wetu. Nami hakika ninaweza kuwasifu ninyi watu wazuri hapa chini, juu ya watoto wenu wapendwa, jinsi mumewaweka wote kwa utaratibu na kadhalika namna hiyo. Mimi . . .

²² U hali gani, Dada? Nami naamini huyu ni, hivi si huyo, mama ndio kwanza aingilie kule nyuma? Bwana akubariki, nina furaha kukuona tena, usiku wa leo. Nami ninaamini huyu ni mke wa Ndugu Willie, hiyo si ni kweli? Na huyo ndiye boshi wa hiyo familia papo hapo, kama ninavyofahamu, kwamba, ama, hivyo ndivyo inavyokuwa katika nyumba yetu.

²³ Na kuwa na nyumba yako, sasa, Paulo alisema hapa, kwa—kwa huyu akida wa Kirumi, wakati alipokuwa . . . Tunaona ya kwamba Paulo alikuwa amepigwa jioni iliyotangulia, iliamriwa na mahakimu, naye alikuwa amepigwa, kwa sababu hakuwa ametenda lolote baya, alikuwa huko juu akihubiri Injili. Nao makasisi pale walimshitaki Paulo, maana alikuwa amehubiri Injili, nao wakasema alikuwa akiupindua ulimwengu juu chini.

²⁴ Ndipo akashuka akaenda mtaani na kulikuwa na maskini mpiga ramli, mwanamke aliyekuwa na ro—roho ya uaguzi, naye aliajiriwa kuwaagulia. Basi walipokuwa wakishuka kwenda barabarani, angemlilia Paulo, na kusema, “Hao ni watu wa Mungu, wanaotwambia njia ya—ya Uzima.”

²⁵ Naye Paulo hakuhitaji huyo ibilisi kumsaidia katika jambo lolote, kwa hiyo aligeuka tu na kuikemea roho hiyo ndani ya mwanamke huyo, basi ilipofanya hivyo, loo, hiyo ikaleta ghasia. Basi walipogundua, huyo—huyo roho alikuwa amemwacha, wala asingeweza kuagua tena.

26 Kwa hiyo, yu—yule aliyekuwa amemwajiri huko nje, na labda alikuwa akimtunza, mbona, ilisababisha ghasia kubwa, nao wakapigwa na kuwekwa gerezani. Nami ninaweza kuwazia Paulo na Sila wakiwa wamelala huko nyuma kwenye gereza hilo lililojaa kunguni kwenye nyua za ndani, huko nyuma kabisa. Huko nje, ambapo wafungwa wazuri kuliko wote waliwekwa, palikuwa pabaya vya kutosha, bali walikuwa upande wa ndani, na walipoenda huko nyuma kabisa, waliwekwa kwenye mikatale.

27 Sijui yeyote... Je, nyote mliwahi kuona mikatale? Nimekuwa na majaliwa ya kuiona, wao—wao wanaiweka katika ninii yako, kuikingama miguu yako, kisha wanaiweka kuikingama mikono yako, kisha wanaiweka kuikingama shingo yako, nawe huyo hapo umeketi pale.

28 Nayo adhabu ya kifo ya Wachina, jinsi walivyokuwa wakiifanya, ilikuwa ni katili sana, wangewaweka kwenye mikatale hiyo na kuweka kidondosha maji, tone moja tu kwa wakati mmoja, likianguka juu ya vichwa vyao, namna *hiyo*, mpaka ikawafanya wawe vichaa. Wangeketi hapo wala wasingewapa chakula wala kinywaji namna hiyo, nayo macho ya—yao yangepinduka na kadhalika, lilikuwa tu, jambo la kuchukiza sana.

29 Wanasema matone machache ya kwanza, bila shaka, kwa labda siku ya kwanza, si mabaya sana, lakini wanasema baada ya siku chache, ya kwamba matone hayo yanasikika kama tani hamsini zikianguka, mwajua, kila wakati, linaangukia mahali pale pale, maana huwezi kusogeza kichwa chako, uko kwenye mikatale hiyo.

30 Basi wazia tu kwamba Paulo na Sila, kwa sababu ya kuhubiri Injili, walikuwa wamelala huko nyuma katika maskini mahali hapo pachafu, na labda panya, na vipanya, wadudu juu yao, na kadhalika. Ni mahali pa jinsi gani kwa mtu anayehubiri Injili! Nasi tunafikiri siku hizi, kwamba tunalalamika kwa sababu tuna mambo yametuwia magumu kidogo; angalieni waliyofanya, na kujua kile kilichokuwa kinawangojea, labda kuuawa kesho yake asubuhi.

31 Lakini walikuwa waaminifu, wa—walikuwa... walidumu waaminifu. Na yapata usiku wa manane mle ndani, nami ninaweza tu kuwazia jinsi hapana shaka walijisikia, migongo yao imeshikamana na huo uchafu wa kale ambamo wafungwa, na katika siku hizo ilikuwa ni ukoma na kadhalika, na kulala kwenye maskini hiyo sakafu ngumu, huenda ilikuwa ni sakafu ya udongo, panya wakikimbia-kimbia juu yao.

32 Lakini katikati ya hayo yote, labda hakuna chakula cha jioni, na kupigwa mpaka walikuwa wakitokwa na damu, na kuchubuliwa, na kuumwa, hakuna daktari wa kuosha hayo majeraha, ama chochote kwa ajili ya maambukizi ambacho

tungetumia siku hizi, ama kitu kama hicho, waliwatupa tu huko nyuma, wakawaweka kwenye mikatale, na kuwaweka katika hali hiyo, lakini hawakuwa wakilalamika. Hakuna hata neno moja la malalamiko lililotoka kwao, huku wakijua, labda kesho yake asubuhi, wangeninii, mahakimu labda wangewaita mbele ya mfalme mkuu na walipofanya hivyo, ama, Baraza la Wazee, nao wangeuawa kwa kuhubiri uzushi huu, ulioitwa siku hizo, Injili, ambayo kweli, kwa bidii tunaishindania imani ile ile siku hizi.

³³ Ndipo tunapoanza kuwazia hilo, ndipo maili zinapungua kidogo kati ya mmoja kwa mwingine, mnaona, kila wakati tunapoanza kuwazia jambo hilo.

³⁴ Ndipo tunaona ya kwamba yapata usiku wa manane, Hapana shaka Paulo na Sila walizungumza juu ya Bwana mpaka yapata usiku wa manane, kisha wakaanza kuimba nyimbo, wimbo mzuri wa kale wa Kikristo. Loo, kama tungeimba leo, tungeimba *Kuna Nguvu Katika Damu*, ama *Loo, Jinsi Ninavyompenda Yesu*, ama kitu kama hicho. Ndipo walipoanza kuimba, mara ghafla, tetemeko la ardhi likapiga mahali hapo. Basi angalia jinsi lilivyofanya, badala ya kuzilundika kuta hizo za jengo hilo kubwa moja kwa moja juu yao, nao . . . na kuwapondaponda hata wakafa, lilizitikisa hizo kuta zikawaondokea, isitoshe, bali li—li—lilivunja na kuwaondolea hiyo mikatale pamoja na hizo nondo, nao wakawekwa huru.

³⁵ Sasa wazia, juu ya miguu yao, juu ya mikono yao na juu ya shingo zao waliwekwa huru, kila mmoja wao. Na badala ya maskini gereza hilo kubwa zito, la Kirumi kuwaangukia, liliangukia mbali nao, namna *hii*, isitoshe, bali pingu na kadhalika zikaanguka. Mnaona, huyo ni Mungu wetu tunaposhikilia kwa uaminifu. Mnaona, hatuna budi kudumu waaminifu. Na maadamu sisi ni waaminifu na—na juu ya . . .

³⁶ Sisi, sasa, huenda tusiwe katika hali kama hiyo, sisi, huenda yeyote asiwe, natumaini hatutakuwa hivyo, bali tunaweza kuwa waaminifu katika yale tunayopaswa kufanya, yale tunayopaswa kupitia, labda ni mateso, labda ni mtu anayekucheka, labda ni mtu anayesema, “Wewe ni wa mtindo wa kale, wewe ni mtakatifu anayejibingirisha,” ama—ama chochote wanachotaka kukuita, ama kukudhihaki, ama chochote kile, hebu na tuwe waaminifu vivyo hivyo, kwa sababu Mungu anaheshimu uaminifu wetu kwa jambo hilo, kama tu vile Yeye alivyokuwa, kuheshimu uaminifu wao kwa kile walichokuwa . . . kilichowabidi kupitia.

³⁷ Ndipo basi, kwa ghafla, wakati yule mfungwa wa Kirumi, ama, yule akida hapana shaka alikuwa—hapana shaka alikuwa, yule mlinzi mlangoni, hapana shaka aliwazia ya kwamba, usiku huo, wakati Paulo na Sila walipokuwa wakizungumza juu ya Maandiko, hapana shaka alijifunza jambo fulani, kwa sababu

hakuwajua hao watu, bali hapana shaka alijua kwa njia fulani, ama kusikia kuimba kwao, ama chochote kile, kilichomfanya ajue, upesi sana, ya kwamba walikuwa ni watu watakatifu.

³⁸ Kwa sababu mnaona, wao... alikuwa ni Mrumi, nao walikuwa ni Wayahudi, naye alikuwa mpagani, nao walikuwa ni Wakristo. Lakini mliona, mara alipogundua kwamba kulikuwa na... ya kwamba gereza lilikuwa limeporomoka, naye alijua ya kwamba ingebidi kuwajibika kwa jambo hilo.

³⁹ Mlinzi, mnakumbuka wakati wa Eliya? wakati alipokuwa amejibadilisha na kukutana na Mfalme Ahabu huko nje, na kusema, “Nilikuwa mlinzi na maisha yangu, bila shaka, yaliwekwa hatarini pamoja na ya yule mtu naye akatoroka.”

⁴⁰ Na—naye akasema, “Vema, utailipia, basi, kwa maisha yako, huo ndio wajibu wa mlinzi.” Kwa hiyo akajifunua na kusema alikuwa ni Eliya nabii, na kusema, “Ulimwacha mfalme aende, Agagi.” Naye akasema, “Uta—utalipa kwa hayo kwa maisha yako mwenyewe,” naye alilipa.

⁴¹ Kwa hiyo basi, tunaona ya kwamba huyu akida wa Kirumi, akijua ya kwamba angejibu kwa maisha yake mwenyewe kwa ajili ya haya, alichomoa upanga wake mara alipogundua kwamba walikuwa wameenda, akaanza kujua, kuuchukua uhai wake mwenyewe, badala ya kulazimika kupitia kwenye adhabu. Baadhi ya wa-... Labda awekwe kwenye mikatale ya aina ile ile, na kadhalika, mpaka atakapokufa, kwa hiyo akawazia angeumaliza tu wote, ndipo akachomoa upanga wake, ajiue.

⁴² Lakini upesi, Paulo alipaza sauti alipoliona, na kusema, “Usijidhuru, kwa kuwa sote tuko hapa.” Mnaona? Ndipo huyo mtu akatambua basi ya kwamba... Hapana shaka kulikuwa na jambo lililotukia kabla ya hapo, ambalo lilimfanya mtu huyu kujua ya kwamba walikuwa ni Wakristo, ama watu watakatifu, kwa sababu upesi alianguka miguuni pao.

⁴³ Ningewazia aliwasikia wakiimba nyimbo, aliwasikia wakishuhudia, alisikia mazungumzo yao. Sasa, hebu tuwazie tu kwa dakika moja, jamani, kama akida huyo wa Kirumi alishawishika na kuhukumiwa kwa sababu aliwasikia hao watu wawili, wafungwa waliopigwa, sasa, sisi tungali huru, wala hatujapigwa wala si wafungwa, lakini kusikia ushuhuda wao kulikuwa na ushawishi mkubwa sana, hata ukamfanya aseme, “Nifanye nini nipate kuokoka?” basi tunapaswa kufanya nini na ushawishi wetu? Mnaona? Tunapaswa kuwa tukishuhudia.

⁴⁴ Ninyi vijana, chochote kile, huenda msihubiri, labda Mungu kamwe hakukuita kuhubiri, bali wewe, kama wewe ni mke wa nyumbani, ama chochote ulicho, tineja, hebu tufanye jambo fulani, mwajua, ambalo, na kuishi maisha yanayowafanya watu kusema, “Vema, huyo—huyo ni Mkristo anayeenda pale, huyo—huyo ni Mkristo.”

⁴⁵ Na kwa hiyo, tunaona ya kwamba jamaa huyu hapana shaka aliguswa kwa njia fulani, kwa hizo nyimbo ama chochote walichokuwa wakifanya mle ndani, kutambua wao walikuwa ni Wakristo. Kwa hiyo akachukua taa, na wakati alipoingia na kuona ya kwamba huyo hapo amesimama Paulo, na hata wafungwa kule nyuma, hakuna mmoja wao aliyekuwa akijaribu kutoroka, kila mtu alikuwa pale, kwa hiyo a—akainua upanga wake, akaanguka miguuni pa Paulo na Sila, akasema, “Mabwana, nifanye nini nipate kuokoka?”

⁴⁶ Sasa, mliona, mimi na wewe siku hizi, na karibu wahudumu wote, ama kadhalika, sikuzote tunajaribu kumwambia mtu *asiyopaswa* kufanya, tungenema, “Sasa achana na uvutaji sigara wako, achana na kusema kwako uongo, achana na wizi wako, acha *hili* lako, ama *lile*.” Sasa, hilo—hilo silo yule mtu alilouliza, ha—hakusema, “Yanibidi *kuacha* kufanya nini nipate kuokoka?” Akasema, “*Nifanye* nini nipate kuokoka?”

⁴⁷ Mnaona, tunajaribu kuwaambia kile wanachopaswa *kuacha* kufanya. Mnaona? Na kusema, “Vema, yanibidi kufanya *hivi, vile, ama vinginevyo*.” La, unaona, hilo silo swali. “Nifanye nini?” si “Niache kufanya nini?” Lakini wewe fanya tu kile unachopaswa kufanya, na hayo mengine yote yatajishughulikia yenyewe, kusema kwako uongo, kuiba, ama—ama kunywa pombe, kucheza kamari, na kufanya mambo maovu, kutakoma wakati utakapofanya yale Paulo alijibia swali lake: “Nifanye nini nipate kuokoka?”

Akasema, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, na ninii yako, na nyumba yako itaokoka.”

⁴⁸ Sasa, sababu ya mimi kuwazia kuhusu kusema jambo hili, kwa sababu ninyi watu hapa, wengi wenu, watoto we—wenu wameokoka, mnaona, wao ni Wakristo. Nimeipenda familia ya Ndugu Evans, vijana hawa hapa. Kwa kawaida, ni tineja yupi ungempata, aketi huku na kumsikiliza mtu fulani, mhubiri akiongea? Mbona, wangukuwa wametoka na kwenda mahali fulani, wasichana wadogo namna huyo.

⁴⁹ Nilimwambia Ndugu Fred, watoto wake, mbona, wa—wanaweza tu kunisikia nikisema jambo moja ambalo ni kosa, wako—wako—wako tayari kuliacha sasa hivi, mnaona; na kuketi kwa heshima ya hali ya juu sana, badala ya kuwa huko nje wakiendesha magari mbio, wakizurura-zurura. Wataninii, watakapokusikia ukinena kuhusu Injili, wako tayari kuketi papo hapo na kusikiliza. Mnaona?

⁵⁰ Sasa, ninajua sote tunataka... tunafikiri watoto wetu ni waasi na mambo kama hayo, lakini la—lazima tukomeshe hayo, na—naamini ya kwamba hatuna budi kukumbuka ya kwamba watoto hawa ndio watoto wazuri kuliko wote ulimwenguni, kwa sababu ni watoto wetu, nasi tunawadai kwa ajili ya Mungu.

⁵¹ Sasa, wokovu wako hautamwokoia mtoto huyo, lakini sasa, Paulo alisema, kasema, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, na yako, na nyumba yako mtaokoka.” Sasa, yeye. . . Sasa, alimaanisha nini kwa hilo? Hakumaanisha ati kwa sababu wameokoka, kwamba nyumba yao ingeokolewa pamoja naye. Alimaanisha hivi: kwamba kwa sababu walikuwa. . . walikuwa. . . kama alikuwa na imani ya kutosha kuokolewa mwenyewe, imani ile ile aliyokuwa nayo kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, ingefanya kazi kwa ajili ya watoto wake. Mnaona ninalomaanisha?

⁵² Sasa, nina watoto wangu, huyo *hapo* mwanangu mdogo, Joseph, Billy, Sarah, Rebekah, vema sasa, ninataka kumwona kila mmoja wao mtenda kazi katika Injili, akifanya jambo fulani, ninataka kuwaona wameokolewa na kujazwa na Roho Mtakatifu.

⁵³ Sasa, nimewakabidhi kwa Mungu na kusema, “Ninamshikilia Mungu kwa ajili yao.” Mnaona? Nami ninaamini wataokolewa, kila mmoja wao. Mnaona? Ninaamini wataokolewa, nami nitakuwa nao Ng’ambo ya pili. Wala—wala siamini wokovu wangu utawaokoa, la, bali imani yangu katika Mungu itawaokoa, mnaona, imani yangu, kumwamini Mungu kutafanya hivyo, na kutawafanya wamjie Kristo.

⁵⁴ Nami ninaamini hapo ndipo ninyi watu, mnawaombea watoto wenu, na hiyo ndiyo sababu watoto wenu wana hi—hiyo adabu, na—na *msichana wa heshima* na *muungwana* halisi katika wakati huu mgumu tunaishi, hata hivyo wana ile—ile sehemu inayowahusu ambayo ndiyo bora sana niijuayo ya watoto wowote. Mnaona? Vema, nafikiri sababu yake ni kwa sababu ya maombi yenu kwa ajili yao, nanyi mumewakabidhi kwa Mungu na mnaendelea kushikilia.

⁵⁵ Mnaona sasa, yule Mrumi alisema, “Nifanye nini?” Alijiulizia tu mwenyewe, akasema, “Nifanye nini?”

Naye akasema, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe, na nyumba yako mtaokoka.” Mnaona?

⁵⁶ Sasa, sasa, tuna jambo moja la kufanya. Hebu turudi nyuma kwa dakika moja tu tupate kitu cha kulishindilia somo langu, sasa, ni hiki: Hebu na tumchukue mzee ninayemjua katika Biblia jina lake Ayubu.

⁵⁷ Sasa, Ayubu alikuwa ni mtu mashuhuri, hakukuwa na mtu kama yeye katika siku zake. Ayubu alikuwa nabii, na watu walikuja kutoka mbali na karibu kumsikiliza Ayubu. Na Mungu alimbariki, naye alikuwa, alikuwa amefanikiwa, alikuwa tajiri, loo, alikuwa na maelfu ya ng’ombe na kondoo, na—na vitu alivyokuwa navyo.

⁵⁸ Na, mbona, alisema wakati angetoka aende mitaani, wale watawala vijana kutoka Mashariki, hao ni wale Mamajusi, wanajimu wenye hekima, mwajua, walikuwa wakisema. . . walisema wangesujudu mbele zake kuomba tu neno la hekima

yake. Mnaona? Alikuwa ni mtu mwerevu, alikuwa—alikuwa ni nabii.

⁵⁹ Na kwa hiyo, ibilisi aliangalia chini, naye akaona ya kwamba—ya kwamba Ayubu alikuwa ni mtu mwerevu. Kwa hiyo nitawaonyesha jinsi mtu mwerevu afanyavyo. Sasa, tukirudi kwenye lile somo, *Yako, Na Nyumba Yako*. Ayubu akasema, alipoona kila kitu kilikuwa tu katika utaratibu mzuri, kama vile nyumba zenu zilivyo sasa, akasema, “Mnajua, watoto wangu wamefunga ndoa na wameondoka, lakini,” kasema, “labda, mmoja wa . . . labda mmoja wao huenda alitenda dhambi.”

⁶⁰ Sasa, kulikuwa na sharti moja ambalo Mungu alikuwa nalo, hilo lilikuwa ni sadaka ya kuteketezwa. Akasema, “Sasa, sininii . . .” Hakuamini watoto wake walitenda dhambi, bali alisema, “Labda wanaweza kutenda dhambi, kwa sababu wanatembeleana, na kwenda kwenye karamu nyumbani mwa mmoja kwa mwingine,” na kadhalika, na kuchanganyikana, nadhani, na kadhalika. Akasema, “Kama mmoja wao ametenda dhambi, kwa hiyo, Bwana, ninaleta sadaka ya kuteketezwa, na kutoa sadaka hii ya kuteketezwa kwa ajili ya mtoto wangu.” Unaona? Na hayo ndiyo yote aliyojua kufanya, hayo tu ndiyo Mungu aliyohitaji, sadaka ya kuteketezwa, hiyo ndiyo, yote aliyohitaji.

⁶¹ Vema, ndipo ile saa kuu ya usiku wa manane ilipokuja na kupiga, naye maskini Ayubu alikuwa katika hali aliyokuwa, yeye, mwajua, alipoteza ng’ombe wake wote, kondoo wake wote, nazo dhoruba zikaja, zikawaua watoto wake, moto ukawateketeza watumishi wake, na—naye aka- . . . afya yake mwenyewe ikadhoofika, naye akaketi kwenye uga wa nyuma ya nyumba juu ya lundo la majivu, na—nao mwili wake mwenyewe ukatokwa na majipu, hata akachukua kipande cha kigae na kuyakwaruza majipu yake. Na hata mke wake akachoka naye akaja na kusema, “Ayubu . . .”

⁶² Sasa, he—hebu kidogo tuwazie tu jinsi alivyosema. Sasa, angalieni yule pale Ayubu ameketi, ameketi huko nje usiku kucha. Hao hapo wafariji wake wameketi wamempa kisogo, nao wamemwambia alitenda dhambi. Huyu ni mfuasi wa kanisa, hiyo ni ha—halmashauri ya mashemasi, ama wowote wale wa kanisa, wakashuka kuja kumwona. Nao wakaketi siku saba pale, na wangali wanamwambia, “Ayubu, afadhali uungame, kwa sababu umetenda dhambi, kwa sababu Mungu hangemwacha mwenye haki ateseke namna hiyo.”

⁶³ Lakini kweli Mungu humwacha mwenye haki ateseke namna hiyo. Mnaona, Mungu, wakati mwingine ma—mambo hutukia kwa sababu tulitenda dhambi, lakini wakati mwingine ni—ni kumjaribu mtakatifu, badala ya kumrudi mwenye dhambi.

⁶⁴ Kwa hiyo, tunaona ya kwamba Ayubu alikuwa ni mtu mwenye haki hata hivyo, naye Mungu alikuwa akimjaribu, kwa

sababu Shetani alisema, “Loo, hakika. . .” alipokuja mbele za Mungu pamoja na wana wa Mungu. Alisema. . .

Kwa sababu Mungu alimwambia, “Umekuwa wapi?”

Akasema, “Loo, kutembea tu huku na huko, na kuzunguka-zunguka huko duniani.”

⁶⁵ Kasema, “Ulimwanzia huyo mtumishi wangu Ayubu? Yeye ni mtu mkamilifu, hakuna mmoja aliye kama yeye duniani.” Mungu alipendezwa na jambo hilo. Loo, Yeye anapenda tu kuwa na mtumishi ambaye anaweza kumtumainia. Akasema, “Hakuna mtu mwingine duniani kama yeye.” Mnaona? Kasema, “Yeye ni mtu mkamilifu.” Na hiyo ilikuwa kabla ya Damu ya Yesu Kristo kumwagwa. Mnaona? Naye akasema, “Yeye ni mtu mkamilifu, yeye ni mwenye haki, ni mwelekevu, hakuna aliye kama yeye.”

⁶⁶ Shetani akasema, “Loo, hakika, angalia kile ulichomfanyia: Umempa kila kitu, anazo nyumba, ana watoto, ana mifugo, ana kila kitu atakacho. Hakika, mtu yeyote angeweza kukutumikia namna hiyo.” Kasema, “Hebu nimchukue wakati mmoja, nitamfanya akukufuru mbele za uso Wako.”

⁶⁷ Akasema, “Shetani, yeye yuko mkononi mwako, lakini usiuchukue uhai wake.” Sasa, hilo lilikuwa ndilo tumaini la Mungu ya kwamba nabii Wake hatampungukia. Mnaona? Naye anatutumainia mimi na wewe, kwamba hatutampungukia.

⁶⁸ Ndipo Yeye, Naye akasema, Yeye, “Usiuchukue uhai wake.” Naye Shetani alifanya kila kitu *ila* kuuchukua uhai wake. Watoto wake wakauawa, na ng’ombe wake wakauawa, na kila kitu kilikuwa. . . utajiri wake wote ukapotea, kisha akapoteza afya yake, na kila kitu *ila* uhai wake, akaketi huko nje na kujikuna majipu yake.

⁶⁹ Ndipo mke wake akaja mlangoni, na—naye Shetani akaingia ndani yake na kusema, “Wewe. . .” Akaangalia huko nje, kasema, “Kwa nini usimkufuru Mungu upate kufa?” Kasema, “Unaonekana mwenye mashaka sana.”

⁷⁰ Akasema, “Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu.” Mnaona? Sasa, kamwe hakusema alikuwa mpumbavu, alisema alinena kama mmoja. Mnaona? Kasema, “Unanena kama mwanamke mpumbavu.” Kasema, “Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; libarikiwe Jina la Bwana.” Mnaona? Kwa maneno mengine, “Nilikuja ulimwenguni uchi,” alisema, “nitarudi uchi; bali Jina la Bwana libarikiwe hata hivyo. Kamwe sikuwa na chochote nilipokuja humu, nami nitaondoka bila chochote; lakini hata hivyo Jina la Bwana libarikiwe.” Loo, jamani!

⁷¹ Mnajua, Mungu atamwacha tu Shetani atujaribu kwa *muda fulani*, kisha anachoka nalo, mnaona. Kwa hiyo, aliona ange- . . . ilimbidi Shetani kumwacha basi. Lakini Bildadi na hao wote

wangali walikaa pale na kusema, “Mbona, ulikuwa mtenda dhambi kisiri.”

Lakini Ayubu akashikilia hili: “Mimi si mwenye dhambi.” Mnaona?

⁷² “Ayubu, umeninii...unafanya...hutaki kuungama,” mnaona, “kwa sababu wewe ni mtenda dhambi kisiri, unafanya hivyo kisiri, na Mungu anakuadhibia hilo, kwa hivyo hiyo ndiyo sababu mambo yanakuendea hivyo.”

⁷³ Lakini akasema, “La, Bwana, mimi si mwenye dhambi.” Kwa sababu alikuwa amesimama imara juu ya haki hiyo ya Mungu, ile dhabihu ya kuteketezwa, alikuwa ameitoa. Hiyo tu ndiyo aliyopaswa kutoa, hiyo tu ndiyo Mungu aliyohitaji.

⁷⁴ Na hivi mliona, Roho wa Mungu akiisha kumjia nabii na kila kitu kikawa sawa, mnaona, Mungu alimrudishia Ayubu nini? Alimrudishia ninii yake... ambapo alikuwa na ng’ombe elfu kumi, akampa ng’ombe elfu ishirini; ambapo alikuwa na kondoo elfu arobaini, akampa kondoo elfu themanini. Mnaona? Naye akamrudishia kila kitu alichowahi kuwa nacho.

⁷⁵ Nanyi mnaona, Hiyo ilisema, “Naye akawarudisha watoto wake saba.” Mnaona? Akampa Ayubu watoto wake saba. Sio, hakumpa watoto wengine saba, bali Yeye alimpa Ayubu watoto wake saba. Sasa, ilikuwa ni nini? Nyumba yake, “Yako na nyumba yako.” Kwa sababu alikuwa mwenye haki, kwa sababu alikuwa amesimama juu ya kila kitu ambacho Mungu alitupa tupate kuwa wenye haki, au, alichompa, kilikuwa ni kutoa dhabihu hiyo ya kuteketezwa.

⁷⁶ Naye alijua ya kwamba Hilo lilikuwa ni Neno la Mungu, wala halingeweza kushindwa. Kwa hiyo, hivi uliwahi kuwazia hao watoto walikuwa wapi? Walikuwa Mbinguni wakimngojea. Mnaona? Yuko pamoja nao leo hii. Naye Mungu akawaokoa watoto wa Ayubu, walikuwa Mbinguni wakimngojea. Mnaona?

⁷⁷ Sasa, kama Ayubu alichukua hatua juu ya jambo lile lile ambalo Mungu alimwambia afanye, jambo pekee lililokuwa apate kuwa mwenye haki, lilikuwa ni kutoa sadaka ya kuteketezwa, hiyo ilikuwa ni haki, Naye akamwokoa Ayubu pamoja na nyumba yake, basi ni nini kilicho haki mbele za Mungu? “Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe, na nyumba yako mtaokoka.”

⁷⁸ Kwa hiyo, kama ninaamini kwa ajili ya nyumba yangu nawe unaamini kwa ajili ya nyumba yako, kwa kuamini hilo, kwamba tunamtumainia Mungu, Mungu huihesabu imani yetu wenyewe, kama alivyomfanyia Ibrahimu, ama Ayubu, ama yeyote wao apate kuwa mwenye haki, mnaona. Kwa hiyo imehesabiwa kwetu kuwa haki, na hivyo ndivyo “Wewe, pamoja na nyumba yako mtaokoka.”

⁷⁹ Loo, nafikiri ni jambo zuri sana. Kwa hiyo basi, isitoshe, bali ninashikilia kwa ajili ya kila ndugu, ndugu zangu wote, dada yangu, sishikili kwa ajili ya hao tu, bali ninashikilia kwa ajili ya kila mtu aliye kanisani mwangu, ninashikilia kwa ajili yenu nyote, nawatakeni mshikilie kwa ajili yangu, kwa sababu ya haki ya imani. Haitubidi kutoa sadaka ya kuteketezwa, Kristo ndiye Sadaka yetu. Lakini inatubidi kuamini sadaka hiyo ambayo Kristo alitoa, ya kwamba Yeye alitufanyia a—ahadi ya namna hii, kwamba “Lolote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, hilo nitalifanya. Mnapoomba, aminini ya kwamba mtapokea mlichoomba, nacho kitakuwa chenu.”

⁸⁰ Sasa, kama ninaomba ya kwamba Mungu atawaokoa hawa watoto matineja, nami ninaamini kwa moyo wangu wote atafanya hivyo, kuona hivyo ndivyo Ayubu alivyosimama. Unasema, “Loo, mwangalie mtoto *huyu*, jinsi anavyofanya.” Sijali mvulana huyo anafanya nini ama msichana huyo anafanya nini, ningali nimemweka mtoto huyo katika mkono wa Mwenyezi Mungu na ninii yangu, “mimi, pamoja na nyumba yangu tutaokoka.” Mnaona? Kwa sababu mimi. . .

⁸¹ Hata ingawa ninaweza kuaga dunia kabla hawajaaga, lakini kwa namna fulani, kabla hawajaondoka hapa, Mungu atawapindua moja kwa moja, huko chini kwenye mkondo, ni—ninaamini hilo, *kwa namna fulani* atalifanya kuwa lenye mashaka sana kwao, hata iwabidi kufanya hivyo. Mnaona?

Na hivyo ndivyo ninavyoamini, ni, “Yako, pamoja na nyumba yako mtaokoka.”

⁸² Nimeona wengi ambao. . . Nimewaangalia hao wakiingia kwenye mikutano yangu. Mara nyingi, maskini mvulana fulani atakuja kule ambaye amekuwa mbaya maishani mwake mwote, yeye, apige magoti na kuanza kulia, asimame, aseme, “Vema, nilikuwa na maskini mama mpendwa, loo, kama yuko Mbinguni usiku wa leo, najua anaangalia chini, naye anafurahia kuniona kwenye madhabahu hii.”

⁸³ Mnaona? Jambo ni kwamba, maskini mama huyo aliomba na kuamini. Mnaona, ameondoka muda mrefu uliopita, lakini haya hapa hayo maombi, kwa sababu ile haki, mnaona, “Wewe, na nyumba yako mtaokoka.” Mungu anajua jinsi ya kufanya kazi, Yeye anajua jinsi ya kufanya, Yeye anajua jinsi ya kufanya kila kitu sawasawa kabisa.

⁸⁴ Kama nilivyosema hivi majuzi, tunapozaliwa kwa Roho wa Mungu, Mungu si dhaifu mahali pamoja na mwenye nguvu mahali pengine, kama una kivuli kidogo cha Mungu ndani yako, chembe iliyo ndogo sana ya Mungu, basi una nguvu zote, una nguvu za kutosha ndani yako kuumba ulimwengu na kutoka nje na kuishi ndani yake. Lakini, bila shaka, nguvu hizo zinatawaliwa na imani, kama sivyo, sote tungekuwa na ulimwengu huko nje, tukiishi ndani yake. Lakini kama wewe

ni mwana wa Mungu, ama binti wa Mungu, una nguvu za Mungu ndani yako. Unaona? Kwa hiyo basi, wewe... Kanuni hiyo hushikilia imani hiyo kwa kitu *fulani*.

⁸⁵ Sasa, hebu tuchukue kwa mfano, sisi sote, tugesema, wakati mmoja tulisema uongo, tungeiba, tunge—tungeaani, na kuapa, na kufanya kila kitu kibaya. Vema, siku moja tulipomkubali Kristo, Yeye alifanya nini? Akawa wazi, mara tulipomkubali; hiyo ni ya imani, kama tu vile Paulo alivyomwambia yule Mrumi awe nayo, aamini, yale hasa Ayubu aliyofanya, aamini. Unaona? Na mara tulipomkubali Kristo kama Mwokozi wetu, papo hapo tukapokea imani ya kutosha, mpaka tukaondoka, hakuna kusema uongo tena, hakuna kuiba tena, hakuna tena udanganyifu. Mnaona? La. Kwa nini? Tulipanda moja kwa moja juu ya dhambi ile tuliyokuwa tukipanda mle ndani; tu—tulihasabiwa imani kiasi hicho kupitia kwake. Kwa nini? Kwa sababu kwamba tunaamini ya kwamba tumeokoka. Hiyo ni kweli? Tunaamini hapa kwamba tumeokoka, kwa hiyo basi tunapanda juu ya hilo, kwa sababu tunaamini tumeokoka.

⁸⁶ Sasa, sikilizeni hili kabla tu sijayafikia yale maswali. Mnaona? Ndugu, dada, nitawapa siri kidogo juu yangu mwenyewe. Mnaona? Nadhani mara nyingi mmeshangaa jinsi ninavyoona maono hayo na kadhalika, kile kinachoyafanya. Ni kwa sababu wakati alipokutana nami usiku huo, na kuniambia hilo, mnaona, ya kwamba jambo hili lingetukia, ninaliamini, ninaliamini kwa uchaji.

⁸⁷ Nami ninaingia kuwaombea wagonjwa, kama ninaweza kupata hisia kwamba jambo fulani liko karibu kutukia, wako karibu kupata afya, kwa hiyo sikuzote, karibu tu sawa. Na hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya na familia yetu, kwa chochote tunachoomba, hatuna budi kuomba, naye Mungu anaihesimu imani, mnaona, kuamini hilo, lazima tuamini kwamba ni kweli.

⁸⁸ Sasa, kwa kipande hicho kidogo cha Mungu, uliposema, “Naam, Bwana Yesu, mimi ni mwenye dhambi, sistahili upendo Wako, bali Wewe ulinipenda kwa hiyo ninakukubali Wewe kama Mwokozi wangu.” Mara, unaondoka moja kwa moja kutoka hapo, na ni kitu gani? Unaachana na kusema uongo kwako, unaachana na kudanganya, unaacha kuiba, unaacha kufanya mambo usiyopaswa kufanya. Kwa nini? Kwa sababu unaamini kwamba wewe ni Mkristo, na kwa sababu unaamini wewe ni Mkristo, unainuka kutoka hapo, unafikia kiwango kingine. Sasa, mnaona?

⁸⁹ Sasa, kama wewe ni mgonjwa, huu hapa uponyaji, wewe amini tu. Sasa, huwezi kujifanya mwenyewe kuliadini, hapana budi liwe ni jambo fulani linakufanyikia, kama tu kuongoka kwako, halina budi kutukia.

⁹⁰ Nilikuwa nikimwambia mke wangu hivi majuzi jinsi nilivyompenda. Kwa hiyo, sidhani anataka nizungumzie jambo hili, lakini ninalifanya faraghani kwa hiyo nadhani ninaweza kulizungumzia hadharani sasa hivi. Nilikuwa nikimwambia jinsi nilivyompenda, na jinsi ambavyo sikuzote nimempenda tangu mwanzo, Nikasema, “Haileti tofauti yoyote. . .”

Akasema, “Loo, Bill.” Alisema jinsi, akizungumzia jinsi alivyokuwa akinenepa, nywele zake zikiingia mvi.

⁹¹ Nikasema, “Mpenzi, unaweza kuwa mpana *hivyo* na usiwe na nywele, ningali ningekupenda vivyo hivyo.” Mnaona? Kwa sababu hapana budi kuwe na kitu fulani pale ambacho huna budi, kimeninii, huna budi kukikuta, kwamba unampenda mtu fulani.

⁹² Na isipokuwa mtu huyo anampenda mtu huyo mwingine. . . Hii ni kwa ajili yenu wasichana wadogo ambao hamjaolewa, mnaona, nanyi wavulana. Unapokutana na msichana huyo unayempenda, na kuna kitu fulani tu unachojua unampenda, na ni hayo tu, ama unampenda mvulana huyo na kwamba, hujali kama yeye ana sura nzuri, ama kama hana sura nzuri, ama kama msichana huyo ana sura nzuri ama hana sura nzuri, hilo halijalishi, bali mnawapenda vivyo hivyo, sasa, afadhali uwe mwangalifu, kwa namna fulani ushikilie karibu pale, kwa sababu hiyo ni kusema, unakaribia nyumbani hapo.

⁹³ Nami. . . ni. . . Ndo—ndoa yenye msingi nje ya hayo hakika itaanguka, la sivyo kamwe haitafanikiwa, kamwe haitakuwa na furaha. Sasa, nilisema hivyo ili kufikia jambo moja ninalotaka kusema: Marafiki, wala wongofu, nje ya kitu kile kile, hautadumu, hautadumu. Unapoenda kanisani, na—nawe unasema, “Vema, nitajiunga na kanisa, nami nitabatizwa.” Kama hayo hayatoki kwenye moyo wa upendo kwa Mungu huko ng’ambo, kamwe hautaenda popote, utaninii tu, yote utakayofanya ni kujiunga na kanisa na kubatizwa.

⁹⁴ Lakini unapoongoka kwa Kristo, upendo kwa Kristo, basi unakusanya imani katika Kristo, kama vile ungefanya kwa mkeo, au kwa mumeo, unakusanya imani hata unatembea katika imani hiyo, sijui, unaninii tu, kitu fulani kukuhusu, una kitu fulani tu kinachokutia nanga hapo, unaona.

⁹⁵ Vema, hivyo ndivyo ilivyo kuhusu Kristo, na yale Kristo asemayo, unayaamini, na unadumu tu nayo. Na hivyo ndivyo, inakuinua tu moja kwa moja juu yake, naye Mungu anaitimiza na kutimiza ahadi Yake, “Kama utamwamini Bwana Yesu Kristo, ninii yako, na nyumba yako mtaokolewa.”

⁹⁶ Kwa hiyo sasa, niliwazia tu ningesema hayo, na ni—nimechukua muda wake mwingi sana, dakika thelathini kusema hivyo. Lakini mnajua ninalomaanisha sasa, hivyo ndivyo ilivyo.

⁹⁷ Kama unaweza kumwamini Bwana Yesu Kristo, sio tu kwa ajili ya wokovu wako mwenyewe, kwa ajili ya wapendwa wako,

kwa ajili ya uponyaji wa mtoto, ama kwa ajili ya mama, ama kwa ajili ya chochote unachotaka kilicho sahihi, nawe unajua kama ulitamani kitu ambacho hakikuwa sahihi, kwanza kabisa hu—hungekuwa na imani ya kutosha kumwomba Mungu, maana unajua si sahihi, unaona, kama wewe ni mwaminifu na unajua ya kwamba ni kweli, basi unaweza kumwomba Mungu kwa moyo safi, ukijua si nia ya kichoyo, na lengo lako na nia yako ni sahihi kabisa, basi unwombe Mungu, na kama mtoto, uamini utakipata nawe unakipata. Sasa, najua hilo.

⁹⁸ Sasa, nilimjia Kristo nilipokuwa na umri wa kama mmoja wa wavulana hawa *hapa*, nadhani, nilikuwa na umri wa kama miaka ishirini, nami ni—nilimtumikia wakati huu wote, nami nina hamsini na miwili, nitakuwa na hamsini na mitatu, siku yangu ya kuzaliwa, nami naweza kusema kwa unyofu ya kwamba sijawahi kumwomba Kristo, kwa uaminifu, chochote, hiyo ni kusema, ni, sasa, ambapo kweli nilimwomba Yeye kwa uaminifu, chochote kilichokuwa sahihi, pasipo Yeye kunipa, ama kuniambia ni kwa nini asingeweza kunipa; halafu baadaye, nikaona kwamba lilikuwa ni jambo zuri sikulipata, mnaona.

⁹⁹ Lakini kumbukeni tu, unapomwamini Yeye, kumwamini, na kumtumaini, usi—usijaribu kujisukuma kufanya hivyo, kaa tu pamoja Naye na kulihoji.

¹⁰⁰ Kama vile wewe . . . kama nilikuwa nikija kwa Ndugu Welch, hapa, kukopa do—dola elfu moja, nadhani nisingeweza kuzipata, maana huenda asiwe nazo, lakini kama alikuwa nazo, na, ni—ningeweza kuzipata. Sasa, ningekuwa na kujaribu kujieleza, ningekuwa niseme, “Welch, nipe elfu moja.” Hiyo siyo njia ya kufanya hivyo. Hiyo siyo njia ya kumwomba Mungu. Ningekuwa huku, ningemwambia Ndugu Welch, ningesema, “Naweza kuzungumza nawe kwa dakika chache, Ndugu Welch?”

“Hakika, Ndugu Branham.”

¹⁰¹ Tuende kando kuketi chini, ningesema, “Ndugu Welch, jambo la kwanza, ninataka kukuuliza: Je, una dola elfu moja ambazo ungeweza kuzipata kwa ajili yangu?”

Vema, yeye, kama yeye . . . sisi—sisi ni marafiki, ama angekuwa akiniomba mimi, ama mimi yeye, ama mmoja wenu ndugu, ingekuwa ni vile vile, tungesema, “Ndiyo.”

¹⁰² “Sasa, hii hapa sababu yake, kile ninachotaka,” ningeyaeleza kabisa na kumwonyesha, niseme, “Ndugu Welch, niko hapa mkutanoni, linanisumbua sana, si—sina budi kuondoka mjini, nami nina deni la dola elfu moja, si—sina budi kupata hizo pesa kutoka mahali fulani, Bwana aliliweka moyoni mwangu kukujia.” Nami ningekueleza. “Sasa—sasa, kutoka kwenye mkutano mwingine niliokuwa nao mahali *fulani*, nina dola elfu moja zinazolingia, ambayo itakuwa yapata miezi mitatu tangu sasa, ninaweza kukulipa, nitakulipa riba juu yake, ukitaka.”

103 Na kuyaelezea tu na kuyaweka wazi, mbona. “Sitaki kuondoka kwenye mji huo namna hiyo, kufanya hivyo ni kujiharibia jina, halafu watasema, ‘Yeye si kitu ila mdanganyifu na *mwizi*, na—na anaondoka mjini akiwa na madeni.’” Mnaona ninalomaanisha? Ninge kuelezea, niketi chini kama ndugu na kulizungumzia pamoja nawe.

104 Vema, ninaamini kama ningefanya hivyo, na—nawe unanipenda jinsi unipendavyo, ungefanya lolote, ungeweka rehani motokaa ama kuuza kitu cha nyumbani upate hizo pesa. Sasa mnaona, ungefanya hivyo, yeyote wenu angefanya hivyo, nami ningefanya hivyo kwa ajili yako.

105 Lakini ingekuwa, ja—jambo sahihi la kufanya ni kuja kuketi chini na kulizungumzia mmoja kwa mwingine, ku—kukujulisha, unaona, kuelezana hisia zetu, “Wewe ni rafiki yangu, hiyo ndiyo sababu nimekuja kwako.”

106 Sasa, hivyo ndivyo ilivyo kwa Kristo, kusema, “Wewe ni Bwana wangu, mi—mimi ni—mimi ni mgonjwa. Mimi. . . da—daktari anasema hawezi kunifanyia lolote, bali—bali ninajua Wewe unaweza, kwa sababu Wewe ni Bwana wangu.” Na—na u—uzungunze tu pamoja Naye mpaka ujisikie basi ya kwamba—ya kwamba—ya kwamba umeupokea, na hiyo ni imani yako, “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.”

107 Nami, ninapojisikia hivyo, ni sawasawa tu na kama ninazo, hakika, ninaendelea mbele, maana nimezipata, mnaona, nimezipata, sasa, Yeye tayari ameniahidi ya kwamba nimezipata, kwa hiyo hilo—hilo latosha, nami ninaendelea tu kushikilia, kungojea, hatimaye, muda si muda mwajua, hizi hapa zinakuja zikitiririka kutoka kwenye ushoroba wa Mbinguni, nawe u—unazo.

108 Lakini hilo ndilo unaloona, “Yako, na nyumba yako mtaokoka.” Na usipowaona wote wameokoka kabla hujaaga dunia, mtaninii. . . watakuwako utakapofika. . . wakati, wakati kule Kuja kuu kutakapokuja, watakuwako.

109 Sasa, mnaelewa ninalomaanisha? Mnaona? Tunafanya kila kitu kwa imani, mwaminini Bwana. Mwamini Bwana kwa ajili ya kazi, mwamini Bwana kutafuta. . . akupe mke unayepaswa kuwa naye, mwamini Bwana kukupa mume unayepaswa kuolewa naye, mwamini Bwana akutumie fenicha mpya, ama kama—kama lile pipa likiisha na ile chupa ikakauka, wala hakuna chakula, nao watoto wana njaa, mwamini Bwana. Mwamini Bwana kwa lolote, unaona, mradi tu ni sahihi, mwamini tu Bwana “nawe utaninii,” unaona, itakuja. Sijawahi kuliona likishindwa maishani mwangu mwote. Mungu awabariki.

110 Vipi kuhusu wewe kunisomea baadhi ya maswali hayo? Ungeweza kunisomea hayo? Na—natumaini nitayapata haya

vizuri. Sitaki kuwaweka muda mrefu sana sasa, kama, labda kama dakika kumi, na—na—na mpatie yeye, Jimmy, muda kidogo wa kuyasoma pale, kuona kama... Nao watakuwa, wataniuliza waziwazi, moja kwa moja, na kwa hiyo, kama siwezi kuyasema, vema mtaelewa.

¹¹¹ Lakini mnaelewa ninalomaanisha sasa, kuamini? “Mwamini Bwana Yesu Kristo, na yako, pamoja na nyumba yako mtaokoka.” Amini kwa ajili yako mwenyewe, na uamini kwa ajili ya nyumba yako, na itakuwa yako. Unasema, “Vema, daktari alisema siwezi kupona.” Vema, kama unaweza kumwamini Bwana, unaweza kupona. “Vema, sina kazi.” Lakini kama utamwamini Bwana, unaona, basi utapata kazi. Na, “Si—sijui la kufanya kuhusu hali *hii* ya mambo.” Mwamini Bwana.

¹¹² Angalia hali yangu ilivyo sasa hivi, na ya mke pale, daima nimewazia Bwana alitaka niondoke Jeffersonville. Sasa, imefikia mahali, hata ikanibidi tu kujikabidhi Kwake, kwa hiyo mimi hapa, Yeye anajua mahali nilipo papa hapa, usiku wa leo, kwa hiyo, na kila mahali anapotaka niende, nitaenda, na yale anayotaka nifanye, nitayafanya, nami nitaendelea moja kwa moja mpaka atakaponiambia, mnaona.

¹¹³ Vema, Jimmy, umeyapata, kijana wangu?

[Ndugu Jimmy Evans anamsomea Ndugu Branham maswali—Mh.]

[Wakati Unyakuo utakapotukia, je, familia zote za waaminio, mke na watoto wataenda? Wako katika imani na wanamtumaini Yesu Kristo kama Bwana.]

¹¹⁴ Naam, naam. **Je, familia yote itaenda katika—katika Unyakuo?** Mnaona, naam. Mnaona? Sasa, kama mkiangalia, Unyakuo utakuwa ni jambo la ulimwengu mzima. Na, je, nyote mlipata somo hilo vizuri Jumapili? Nyote mnalielewa vizuri, kuhusu jinsi tulivyo karibu kwenye wakati huo, *Yale Majuma Sabini Ya Danieli?*

¹¹⁵ Nyote mlikuwapo Jumapili, siyyo? Naam. Vema. Vema, nafikiri, Ndugu Welch, una kanda yake, na baadhi yenu mngeweza kuicheza. Na—nanyi mna ramani yake, naamini, siyyo? Nanyi mwichore tu, na—na, kwa wale ambao hawakuwa hapa, labda muwaelezee, mnaona, ili wa—waweze kulipata. Ninawatakeni mwone kwa Maandiko tu kwamba sina hata neno moja la kusema juu yake, Maandiko yanalithibitisha tu jambo hilo, ya kwamba tuko—tuko katika wakati wa mwisho.

¹¹⁶ Sasa, tulikuwa tukizungumza leo, hao ndugu. Unasema, “Vema, Ndugu Branham, kama unaamini ya kwamba Unyakuo umekaribia hivyo, basi kwa nini unaenda kuvua samaki?” Kama nikiweka nia yangu kwake sikuzote, karibu ingekutia wazimu, unapowazia juu ya makumi elfu ya watu huku nje katika dhambi ambao hawamjui Kristo, nami ninawazia kwamba “Mimi hapa, nifanye nini?”

¹¹⁷ Lakini hivi ndivyo ninavyowazia: siwezi kumwokoia mmoja isipokuwa Mungu aliwaita. Mnaona? Siwezi kufanya hivyo, wala nisingeweza kuwaokoa kwa vyovyote vile. Lakini, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Kwa hiyo kama Yeye haniambii niende wapi, basi nifanye nini? Mnaona?

¹¹⁸ Kwa hiyo, jambo ninalofanya, ni kuto—kutochoka kabisa kulihusu, hilo lingekuwa baya zaidi ya hapo awali, Ninafurahia jambo hilo, nime—nimeandaa yote na niko tayari, mwajua, “Atakapokuja, Bwana, mimi hapa.” Ninangojea tu.

¹¹⁹ Na sasa, hili ndilo linalotukia: Wale—wale watakatifu walionyakuliwa, kama mlivyoona kwenye ile chati Jumapili . . . Sasa, wale ndugu wa mwanzoni wa Kipentekoste, ama, marehemu ndugu wa Kipentekoste hawakuyapa yale, yale makanisa ya nyuma nafasi ya kutosha kule, siamini. Lakini ninaamini ya kwamba kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili . . . Nasi tunazaliwaje mara ya pili? Tunapomwamini Bwana Yesu Kristo, mnaona, na kukubali . . . Sasa, siamini kwa sababu tu unasema niani mwako, unaamini, ninaamini maisha yako yanaonyesha kama wewe kweli ni Mkristo au la. Mimi . . . Unasema, “Nini . . .”

¹²⁰ Leo hii, huyo mama kule chini, alisema *jambo fulani* kuhusu kuwa M—Mkristo ama *chochote kile*, naye akasema, “Na ni dhehebu gani?” Mnaona, upeşi sana wanataka kujua ni dhehebu gani.

Nikasema, “Si mfuasi wa dhehebu lolote, Mkristo tu.” Mnaona?

¹²¹ Mkristo, unasema, “Vema, *Mkristo* maana yake ni ‘Mkambeli.’” La, hilo ni—hilo ni . . . wanawaita tu, “Mkristo,” bali hilo halimaanishi “Mkristo.” Ninawajua watu wengi ambao ningewazia ni wafuasi wa lile lililoitwa Kanisa la Kikristo ambao hawakuwa Wakristo. Na wahudumu Wakristo watakwambia jambo lile lile la Kanisa la Kikristo, kwamba wana wafuasi wengi ambao si Mkristo.

¹²² Lakini *Mkristo* si kanisa unaloshiriki, ni tukio ulilopata la kuzaliwa katika familia ya Mungu.

¹²³ Sasa, angalieni katika jambo hilo, Unyakuo utakuwa wa ulimwengu mzima, kwa sababu Yeye alisema, “Wawili watakuwa kondeni, nami nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja. Kutakuwa na wawili kitandani, nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja.” Mnaona, wakati kukiwa giza upande mmoja wa dunia, ambako kuna wawili kitandani, utakuwa ni wakati wa mavuno upande wa pili wa dunia ambako kutakuwako na wawili kondeni. Mnaona? Na inaonyesha kutakuja Unyakuo mmoja mkubwa mno, utatoka moja kwa moja kutoka ulimwenguni. Mnaona? “Wawili kondeni, nami nitamchukua mmoja, nimwache mmoja. Wawili kitandani, nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja.”

124 Sasa, tu—tunaona ya kwamba...Ndipo basi kila mtu aliyeonekana ameandikwa katika kile Kitabu alikombolewa katika Siku hiyo, kabla ya ile dhiki. Kwa hiyo, kama watoto wako, mama yako, wapendwa wako, wowote wale, kama jina lao limeandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, watoto wangu wa thamani, mtakuwa papo hapo.

125 Haidhuru tuko wapi, kama—kama mimi, nikiruka kwenda ng'ambo, na—nayo ndege ilipuke hewani pamoja nami, msipate hata kipande kimoja changu katika mwili huu, hilo halitakuwa na uhusiano wowote nao. Mnaona? Nitakuwa pale pale vivyo hivyo. Msijali kuhusu hilo, nitakuwa papo hapo kuwapa mkono na—na kumsifu Bwana pamoja nanyi, kumvika taji kuwa Mfalme wa mfalme na Bwana wa bwana. Mnaona?

126 Nadhani labda, kuhusu mwili wa Paulo, hakuna hata chembe ya vumbi iliyosalia, karibu hivyo, lakini nyenzo zote zilizoufanyiza mwili wake ziko mahali fulani, kwa hiyo zitakusanywa pamoja siku hiyo.

127 Unapokufa, kwa kweli hufi, Mkristo hawezi kufa, hakuna kitu kama kifo kwa Mkristo, si katika Biblia.

128 Kama vile wakati Lazaro, Yeye alisema...walisema... "Rafiki ye—yetu Lazaro amelala," Yesu alisema. Mnaona, Yeye kamwe hakusema alikuwa amekufa, alisema, "Analala."

Wakasema, "Loo vema, kama analala na—nadhani anaendelea vizuri basi, yeye, lazima anaendelea vizuri zaidi."

129 Kwa hiyo ilimbidi kuzungumza lugha yao, akasema, sasa, vinginevyo, "Kwa lugha yenu wenyewe, amekufa. Nami nina furaha kwa ajili yenu," kwamba Yeye hakuwako, "Nitaenda, na kumwamsha." Mnaona? Loo, naam. Mnaona? Kulala, mnaona Yeye angali alikuwa na walio Wake, mnaona, "Kwa ajili yenu, kwa njia yenu ya kujua, amekufa, lakini Kwangu, amelala, wala Mimi siendi—siendi kumfufua, ninaenda tu kumwamsha." Mnaona? "Ninaenda kumwamsha."

130 Na kwa hiyo, m—mnaona wakati Yesu, Mwenyewe, alipokufa...Mnaona, kuna sehemu tatu za mwili, uh, kwa hiyo, uh, kwa sehemu tatu zetu, nafsi, mwili, na roho, kama mlivyoona zile *Nyakati Saba za Kanisa*, nilizichora; milango mitano ya kuingia mwilini, kuona, kuonja, kugusa, kunusa na kusikia; na dhamiri, na kadhalika, kwa nafsi; na—na halafu kwa roho, kuna njia moja, hiyo ni hiari yako mwenyewe ya kujichagulia, hiyo ni "kufanya uamuzi," unaona, unaweza kulikataa ama—ama unaweza kulikubali.

131 Na kwa hiyo sasa, mtu anapomkubali Kristo na ameokoka, nyumba yako yote, familia yako yote, kila familia ya duniani itaokolewa, sasa, wakati, ama, kuingia.

132 Wakati Kristo alipokufa, Yeye alimkabidhi Mungu Roho Wake kabla ya kuondoka m—msalabani, alisema, "Mikononi

Mwako naiweka Roho Yangu.” Nayo Biblia ilisema Nafsi Yake ilienda kuzimuni na kuhubiri, hiyo ni dhamiri Yake na Kile alichokuwa, kwa roho zilizokuwa kifungoni nao mwili Wake ukaenda kaburini.

¹³³ Sasa, mnaona, Yeye alikuwa nyuma ya kizuizi cha Maandiko, asingeweza kufufuka kwa siku tatu. Nayo Roho Yake ilikuwa imerudi *hapa* juu Uweponi mwa Mungu. Sasa, baada ya siku tatu, Kizuizi hicho kiliondolewa, kwa sababu Maandiko yalitimizwa, ndipo Roho Yake ikaenda kwa Nafsi, nayo Nafsi ikaenda kwenye mwili, akafufuka. Alisema kabla hajafa, Yeye alisema, “Ninao uweza wa kuutoa uhai Wangu, ninao uweza wa kuutwaa tena.”

¹³⁴ Sasa wazia jambo hilo, kila mmoja wenu humu ndani, nijuavyo mimi, usiku wa leo, ni Wakristo, sasa angalieni, kile Kitu kilicho ndani yako sasa, Roho aliye ndani yako sasa, ni Roho yule yule atakayekufufua. Unao uweza wa kuutoa uhai wako, unafanya hivyo sasa hivi kwa ajili ya Kristo, halafu unao uweza wa kuutwaa tena. Unaona? Unao uweza wa kuutoa, na uweza, wa kuutwaa, kwa kuwa ni Roho yule yule wa Mungu aliye ndani yako ambaye anakufufua, ni Roho yule yule wa Mungu aliyekuwa ndani ya Kristo aliyemfufua. Kwa hiyo una uweza wa kuutoa, una uweza wa kuutwaa.

¹³⁵ Na unapokufa, au, nawe, wapendwa wetu, ama mtu fulani anapotutangulia, hawajafa, roho yao iko pamoja na Mungu, nafsi yao iko chini ya madhabahu ya Mungu, mwili wao uko kaburini, nao wanajua mahali ulipo hasa.

¹³⁶ Kwa hiyo, ni jambo gani linalotukia? Wakati Maandiko yote yametimia, kama katika Biblia ilisema, “Nafsi hizi ziko chini ya madhabahu, zilikuwa zikilia, ‘Bwana, hata lini, hata lini?’” Wanataka kurudi duniani na kuwa katika miili. Akasema, “Bado muda kidogo tu, mpaka watumishi wenzenu wameteseka kama vile mlivyoteseka kwa ajili ya ushuhuda wa Kristo.”

¹³⁷ Ndipo unaona wakati Maandiko hayo yatakapotimia, basi hizo roho zinashuka moja kwa moja, moja kwa moja chini ya madhabahu pale na kuichukua nafsi hiyo, nafsi hiyo inashuka moja kwa moja na kuuchukua huo mwili, nawe huyo hapo, umefufuka tena. Wazienu jambo hilo, Roho Mtakatifu ambaye yuko moja kwa moja katika jengo hili usiku wa leo, Roho Mtakatifu aliye papa *hapa* moyoni mwangu, atanifufua katika siku ya mwisho.

¹³⁸ Roho Mtakatifu huyu aliye ndani yangu sasa, atahakikisha ya kwamba nina mwili mchanga, usiopatikana na mauti na wala kamwe hautaenda. . . Roho Mtakatifu aliye ndani yako, atahakikisha kwamba mvi zitatoweka na chochote kile. Nawe, na uzee, kama wewe ni mzee *sana*, na masharubu yananing’inia, na unatembea namna *hiyo*, haileti tofauti hata kidogo, Roho Mtakatifu yeye yule aliye ndani yako atakubadilisha upesi sana

kwenye Siku hiyo, uwe tu kijana mwanamume na mwanamke; hiyo ni Biblia. Hiyo ni kweli.

139 Roho aliye ndani yetu sasa hivi, sasa hivi, si Yule *atakayekuja*, Yule aliye ndani yetu *sasa*. Ni Mungu ndani yako sasa. Naye atafufua . . . Unaweza kujifufua mwenyewe. Basi kwa nini huwezi kufanya hivyo sasa? Kwa sababu, unaona, kuna Maandiko yanayoshikilia, huna budi kungojea mpaka kule Kunyakuliwa.

140 Unaona, haya basi, huna budi kukaa papo hapo. Unaona? Huruhusiwi kupanda juu *hivi*, kama ingeruhusiwa, mbona, tungeninii, nilisema, tungejijengea ulimwengu mdogo wa kibinafsi, ungukuwa ukiishi kwenye ulimwengu mmoja, nami kwenye mwingine, na basi kusingekuwako na Kuja kwa Bwana Yesu. Basi ingekuwa ni kitu gani? Unaona?

141 Lakini una uweza wa kufanya hivyo. Kivuli kidogo kabisa cha—cha Mungu kingeweza kufanya lolote, maana mnaona, Yeye—Yeye ni mwenye nguvu zote. Mnajua kile *mwenye nguvu zote* . . . ? Yeye hana kikomo, hana kikomo, hana kikomo na yuna nguvu zote. Hiyo ni *kutokuwa na kikomo*, hakuna tu, vema, hu—hu—huwezi kulielezea, unajua. *Pasipo na kikomo*, ni kama tu kwenye kamera, pasipo kikomo, ni kutoka tu *hapo* na kuendelea. Halafu *mwenye nguvu zote* ni “mwenye uweza wote.” Yeye sikuzo- . . .

142 Nikisimama huko nje, na kuangalia kupitia kioo, nami ningeweza kuona miaka milioni mia moja na ishirini ya anga la nuru, wakati yule—wakati yule mnajimu aliponipandisha huko juu kuangalia, akaniaacha niangalie kupitia kioo hicho kikubwa usiku huo, ningeweza kuona miaka milioni mia moja na ishirini ya anga la nuru.

143 Vema, ukizungumza juu ya Jupita na Mirihi na nyota hizi unazoziona sasa, vema jamani, wazia kile mia moja na . . . Nuru husafiri karibu, ni ngapi? Themanini . . . ? Maili mia moja, themanini na sita elfu kwa sekunde, maili mia moja na themanini na sita elfu kwa sekunde, na kuchukua miaka milioni mia moja na ishirini. Whiu! Kwa sekunde moja, mia moja na themanini na sita elfu, basi ivunje ifikie miaka milioni mia moja na ishirini. Basi unapata nini? Hizo ni maili. Loo, jamani! Inatufanya tu kujisikia kana kwamba mna—mnaninii tu . . . Mnaona?

144 Lakini sasa, na kisha mbele ya huko, kuna mwezi na nyota nyingi tu kama kulivyokuwa . . . Naye anazishikilia kwa nguvu za Neno Lake Mwenyewe. Na Kitu kile kile kinachozishikilia kiko ndani yako kama Mkristo. Loo, jamani! Mnaona, mnaona, haya basi. Kwa hiyo hapo, hivyo ndivyo ulivyo.

145 Unaona, watu hujaribu kuwazia, “Vema, mimi ni Mkristo, nakisia itanibidi kudunishwa kila mahali.” La, sivyo. Wewe ni Mkristo, ndugu! Hiyo ndiyo ninii ya juu . . . Wewe ni mwana wa Mungu. Baba yetu ni Mfalme, bila shaka. Amina. Naye Baba

yetu, akiwa ni Mfalme, sisi ni—sisi ni wanawe, sisi ni wana na binti za mfalme, amina, wa Mfalme. Mnaona? Kilicho juu sana, cha juu sana kinachoweza kuwa, Roho mwenyewe wa Mungu wetu yuko ndani yetu. Jambo ndilo hilo.

¹⁴⁶ Kwa hiyo, tunajali nini kuhusu yale yanayotukia hapa? Mnaona, Hapo ndipo Mahali panapofaa, huu ni wakati tu wa kujaribiwa, wakati Baba atakapomaliza, hebu twende, hebu twende Nyumbani. Mnaona? Kwa hiyo, inaleta tofauti gani?

¹⁴⁷ Kwa hiyo basi katika hilo, mwaminio wa Bwana Yesu Kristo, kama watoto wako hawajaokoka, mpaka watakapookoka. Naye Yesu alisema, sasa, kumbukeni, Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni.”

¹⁴⁸ Basi asipokuja Hukumuni, anaenda wapi? Katika Kunyakuliwa. Mnaona? Maana hiyo ndiyo Hukumu baada ya Kunyakuliwa. Mnaona? “Hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Kwa sababu amemwamini Bwana Yesu Kristo. Hilo si ni zuri sana? Kwa hiyo wao, watoto wenu watakuwa kule pamoja nanyi, wapendwa wenu watakuwa kule pamoja nanyi, nami natumaini niko kule pamoja nanyi. Amina.

¹⁴⁹ Vema, una lingine hapo, Jamani Jimmy?

[Tunafahamu ulimwengu uliumbwa kwa imani. Waweza kueleza kidogo kuhusu imani?]

¹⁵⁰ Ulimwengu uliumbwa. Sasa, katika Waebrania tunaona ya kwamba, twafahamu ya kwamba ulimwengu uliumbwa kwa—kwa vitu visivyoonekana.

¹⁵¹ Sasa, nita—nitajaribu kuharakisha, maana sikuyaona hayo yote madogo, hayo maswali yote pale. Sasa, hebu tuchukue tu, turudi nyuma kwenye ziara ndogo. Na—na tayari ni saa nne, nami nilimwambia Mama ningekuwa tayari kwenda ifikapo saa nne. Je, m—mmeshikwa na usingizi sana hata hamwezi kungojea kwa dakika moja tu, ama, mmechoka kupindukia? Mnaona?

¹⁵² Vema, angalieni, kabla hapajakuwapo na chochote, hebu tuone, kabla hapajakuwapo na nuru, kabla hapajakuwapo na ulimwengu, kabla hakujakuwako na nyota, kabla hakujakuwako na atomi, kabla hakujakuwako na molekuli, kulikuwako na Mungu. Mtu huyu ni nani, Mungu? Yeye ni hewa, Yeye ni nuru, Yeye ni...? Yeye ni Mungu, hayo tu ndiyo yote unayoweza kusema. Unaona?

¹⁵³ Wazia tu, molekuli, kuna katika atomi moja ndogo, kuna molekuli *kadhaa*. Mnaona? Na kisha mbele zaidi ya molekuli, kabla hata hapajakuwapo na moja ya hizo, bado kulikuwako na Mungu. Alikuwa yote, alijaza kila kitu. Mnaona?

¹⁵⁴ Sasa, katika Mungu huyu, sasa, tunaenda—tunaenda kumfanya Yeye Umbo do—dogo ili mweze kuona, sasa, ndani ya

huyu—Mtu huyu Mungu, huyu ndani ya—ya Mtu huyu kulikuwa na, kulikuwa na sifa, na hizo sifa zilikuwa ni kuwa Baba, zilikuwa ni kuwa Mponya, zilikuwa ni kuwa Mwokozi; hizo ndizo zilizokuwa katika Mtu huyu mkuu, sasa, Hiyo ilikuwa kabla ya molekuli ama chochote kile, wakati hapakuwapo na molekuli, bali bado kulikuwako na Mungu.

¹⁵⁵ Sasa, mle ndani kulikuwa na sifa za kuwa Baba, kuwa Mwana, kuwa Mwokozi, kuwa Mponyaji, kuwa vitu hivyo vyote. Sasa, Mtu huyu aliye na hii . . . Sasa, kama Mtu huyu, Mungu . . .

¹⁵⁶ Sasa, yale aliyofanya, jambo la kwanza, hebu tuseme aliumba, kadiri tujuavyo, iliyo ndogo sana tunayoweza kuivunja, ilikuwa ni molekuli. Na baada ya Yeye kufanya molekuli, Yeye alifanya bilioni mia moja ya hizo katika sekunde moja. Ninii tu, Yeye alifanya nini? Yeye aliinena ikawa. Na sasa, ninyi . . . Hapa kungekuwa na somo zuri papa hapa, kama tu tungalikuwa na wakati wa kuliingilia. Mnaona?

¹⁵⁷ Sasa, Yeye aliinena, na aliposema ziwepo, molekuli zilianza kuzunguka. Kisha akasema, “Na kuwe na atomi.” Na kuna kanuni za atomi, na bado zinadumu katika kanuni hiyo, zingali zinasafiri, kila kitu kinasafiri katika sheria za Mungu.

¹⁵⁸ Kama vile yule mtu niliyekuwa nikiwaambiwa habari zake, mimi na yule jamaa mzee Ndugu Banks Wood tulishuka, mwajua, kwenda kumwona. Alikuwa akizungumza kuhusu . . . “Vipi . . .?” Nilimwuliza, yeye alikuwa ni kafiri, nami nikamwuliza, “Utomvu huo unaondokaje kwenye huo mti Agosti, na kuingia chini mizizini? Ni kitu gani kinachoufanya ufanye hivyo?” Yeye . . . “Ni kitu gani kinachoyafanya majani yawe kahawia?”

Akasema, “Kwa sababu utomvu . . .” akasema.

“Kwa nini—kwa nini utomvu unashuka?”

Akasema, “Vema, unaninii tu, unashuka.”

Nikasema, “Vipi kama hautashuka chini?”

Kasema, “Huo mti ungekufa.”

¹⁵⁹ Nikasema, “Vema, ni Akili gani inayoufanya utomvu huo uingie chini mizizini? Hebu weka ndoo ya maji kwenye nguzo uone kama yatashuka Agosti.” Mnaona? Nikasema, “Ni Akili gani inayoufanya utomvu huo uondoke kwenye huo mti na kushuka chini mizizini? Kitu fulani huuambia ushuke kule chini, la siyvo utaganda na kufa, mti huo utakufa.” Mnaona? “Wala hatujawa na hali ya hewa baridi wala chochote kile bado. Lakini una . . .”

Akasema, “Vema, ni—ni maumbile tu.”

“Vema—vema, maumbile ni nini? Niambie maumbile ni nini.” Mnaona? Maumbile ni kanuni ya Mungu, naam, ni kanuni ya Mungu.

160 Sasa, imani ni kanuni ya Mungu, mnaona, jambo lile lile. Nguvu hizi zote za Mungu tunazozungumzia tunazifikia kwa imani, “Mambo yote yanawezekana. Uambie mlima huu, ng’oka, wala usiwe na shaka moyoni mwako. Amini uliyosema, yatatimie, yatakuwa yako.” Kufikika, kama una kanuni, hiyo hapo, unaona, hiyo kanuni ni imani inayotawala mambo yote.

161 Sasa, Mungu kwa kanuni Yake, alifanya molekuli, hiyo ni kanuni ya Mungu, ndipo Mungu akafanya atomi, kisha kutokana na hizo, Mungu akafanya jua, kutoka kwa hilo, kutoka kwa jua akafanya nyota, kutoka kwa nyota. . . (Hivyo ni vipande vidogo vya jua vikiruka.) Alikuwa na nini? Huko nyuma kabisa kuna sifa Zake zikijionyesha zenyewe.

162 Ndipo ukaja ulimwengu, na baada ya ulimwengu ukaja uumbaji, na baada ya uumbaji, ikaja kanuni ya uumbaji. Baada ya kuwepo ulimwengu. . . Ni kitu gani kinachoufanya ulimwengu huu? Mtu yeyote anawezaje kulielezea? Hebu zungusha mpira vyovyote utakavyo, utupe hewani, hautazunguka mara mbili, na kufanya mizunguko bilioni moja kwa sekunde, hautazuguka mara mbili mahali pamoja, na hata hivyo, tuna taarifa ya miaka elfu sita, ulimwengu huu haujawahi kukosa wakati wowote, ukizunguka saa ishirini na nne sawasawa kabisa, bila kusimama mahali popote. Mnaona?

163 Ni kitu gani hicho? Mtu huyu mkuu, kabla hapajakuwapo na ulimwengu. . . Kabla ulimwengu haujakuwapo, huyo ndiye yule Mtu mkuu mle ndani, kanuni ya Mungu ikiufanya upinduke. Kanuni iyo hiyo ya Mungu, Yeye aliunena tu ukawa, Yeye ni Muumba, Yeye huumba. Mnaona? Na hiyo ndiyo sababu ulimwengu uliumbwa pasipo. . . Kwa imani, Mungu aliumba ulimwengu, kwa sababu imani Yake Mwenyewe, unaona, iliumba ulimwengu. Na hivyo ndivyo. . .

164 Sasa, Yeye, ama, mnaona, Yeye alishuka akiumba mwanadamu na wanyama wote, mpaka alipoifikia dhambi, bali asingeweza kuumba dhambi, kwa sababu Yeye hawezi kuwa mwenye haki na Baba wa haki, kisha aumbe dhambi. Kwa hiyo mnajua alilofanya? Alimfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe, huku akijua ya kwamba angeanguka, bali akamweka kwenye msingi wa uhuru wa kujichagulia, Akasema, “Sasa, usiuguse mti *huu*.”

165 Sasa, Yeye asingeweza kusema. . . Sasa, Yeye alijua angeugusa, bali asingeweza. . . ? . . . yeye kuugusa, kwa sababu Yeye alisema, “Uguse Mti *huu*, upate kuishi, unaweza kuugusa mti *huu* na ufe.” Mnaona?

166 Naye alijua mwanadamu angeshindwa, bali hata hivyo asingeweza kumfanya ashindwe, ilimbidi kufanya hivyo kwa ninii yake. . . kwa—kwa hiyo hilo linamfanya Mungu kuwa mwenye haki, mnaona, mwanadamu alianguka mwenyewe.

Baada ya Yeye kumfanya awe karibu sana na Yeye, alimweka kwenye msingi wa uhuru wa kujichagulia, na kwa hiyo, hapo ndipo alipoangukia, kwa tendo lake mwenyewe la uhuru wa kujichagulia alianguka.

¹⁶⁷ Na leo hii, kila mmoja wenu ninyi watoto, na kila mmoja wetu sisi watu wazima amewekwa karibu na miti iyo hiyo miwili, tunaweza kuukubali Uzima, ama kuukataa. Mnaona? Kwa hiyo Mungu aliunena tu ukawa, nao ulimwengu ukaumbwa, sakafu ii hii ni Neno la Mungu, kitu hiki *hapa* ni Neno la Mungu, miili yetu ni Neno la Mungu, na kila kitu kilichopo, ni Neno la Mungu, mnaona, kwa sababu yote yalitokana na Mungu.

¹⁶⁸ Vema, bwana. Sasa—sasa, kama hilo si kweli, kama hilo halilielezei, mbona, u—unaweza kuniandikia waraka, ulete kanisani, ukitaka.

¹⁶⁹ Vema, Ndugu Jimmy.

[Wakorintho wa Kwanza 16:22, fafaua.]

¹⁷⁰ Hebu tuone, Wakorintho wa Kwanza 16:22. Vema, bwana, hebu kidogo. Masomo ha—haya ma—madogo katika Maandiko kweli yangeweza kutusaidia. Yangeweza—yangeweza kuwaimarisha na kuwafanya—kuwafanya watu wakuu, wenye nguvu.

¹⁷¹ Ulisema kumi na sita, mwanangu? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “. . . na awe . . .” Loo, jamani, sijui kama ninaweza kutamka jina hilo au la. A-n-a-t-h-e-m-a M-a-r-a-m-a-t-h-a. Mtu mmoja aliye na Biblia nyingine, angalia jinsi lilivyoelezewa. Hilo *anathe*— . . . Ati nini? Inaonekana kama hivyo ndivyo. Ni kitu gani, Fred? Chukua, chukua nyingine, kuna mtu aliye na Biblia nyingine? Angalia kama liko mle ndani.

¹⁷² Anathema. Vema, *anathema* ni nini? Sasa, mmenipata. Unajua, Fred? Mtu yeyote, yeyote wenu ninyi nyote anajua *anathema* ni nini? Una kamusi? Tunaweza kulipata katika dakika moja tu, leteni kamusi.

¹⁷³ Vema, wakati anapoitafuta hiyo, labda ninaweza kujibu lingine. Vema, Bwana.

[Fafaua, “Nilimwona Shetani, katika umeme, akianguka kutoka Mbinguni.”]

¹⁷⁴ “Nami nilimwona Shetani akianguka kutoka Mbinguni kama umeme.” Hapo katika Luka ndipo . . . inatoa Andiko pale? Ninii tu, vema, nadhani hivyo ndivyo ilivyo.

¹⁷⁵ “Nilimwona Shetani akianguka kutoka Mbinguni kama umeme.” Sasa, hilo, sasa, nitaeleza tu hili kwa urahisi, na kama halitoshi, basi ninyi—nijulisheni tu, nami nitaelezea kwa utondoti. Mnakumbuka . . .? Tuta—tutalipata hilo tutakapoingia, mbele zaidi katika Maandiko kwenye somo letu kule katika hilo.

¹⁷⁶ Mwajua, Yesu, hiyo ilikuwa mara tu baada ya Yesu kuwapa wanafunzi Wake nguvu dhidi ya pepo wachafu, nao wakatoka wakiwatoa pepo. Aliwatuma wawili wawili, Naye akasema, “Msiende kwa Mataifa, bali afadhali mwende kwa kondoo wa Israeli waliopotea. Na katika kuenenda kwenu, uhubirini basi Ufalme wa Mbinguni; na kuwaponya wagonjwa, na kutoa pepo,” na kadhalika. Vema, basi, halafu, wakarudi wakishangilia, kwa furaha (Sasa, ninyi mliouliza hilo swali mnajua hapo ndipo lilipo, mnaona.), wakarudi kwa furaha wakishangilia. Naye akasema—Naye akasema, “Msifurahi kwa sababu majina yenu, uh, msifurahi kwa sababu pepo wanawatii, bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa Mbinguni.” Akasema, “Nilimwona Shetani akianguka kutoka Mbinguni kama umeme.”

¹⁷⁷ Mnaona, nguvu za Kanisa hilo zikisonga mbele zilikuwa tu zimeuvuruga ufalme wote wa Shetani, mnaona. Naye akamwona wakati akianguka kutoka mahali pake ni kwa sababu Mungu alikuwa tena amelipa Kanisa Lake nguvu kwenda kunini... Alimwona akianguka kama umeme kutoka Mbinguni. Alitupwa moja kwa moja kutoka mahali patakatifu na kila kitu, mnaona, kwa nguvu za ha-...nguvu hizo za Kanisa hilo, wao wakiwa na nguvu. Yesu alisema, “Nimewapa mamlaka juu ya pepo wachafu.” Mnaona? Nao kweli waliuvuruga ufalme wa Shetani. Tungeweza kufanya nini nayo leo? Loo, Bwana asifiwe!

¹⁷⁸ Vema, Ndugu Jimmy, labda una lingine?

[Fafanua, “damu kwenye hatamu ya farasi,” katika Ufunuo.]

¹⁷⁹ Vipande vya hatamu, ile Har-Magedoni, uh-huh, katika Ufunuo. Sasa, katika siku za mwisho, tunafikia mahali ambapo Tito, katika mwaka wa 70 A.D., aliziteka kuta za Yerusalemu, na kuzibomoa kuta za Yerusalemu. Wanadai ya kwamba kulikuwa na damu nyingi sana iliyomwagika miongoni mwao, moja kwa moja kwa Wayahudi milioni moja au zaidi waliokuwa ndani ya hizo kuta, mpaka wakawaua hata wanawake, watoto wachanga, vema, ilikuwa ni mbaya sana mpaka wakaninii...

¹⁸⁰ Walikuwa wamemkataa Roho Mtakatifu. Mnaona sasa, Mungu, wakati Yeye...Wakati walipomkataa Kristo na kumwita Beelzebuli, Yeye alisema, “Ninawasamehe kwa hilo,” mnaona, “nitawasamehe, lakini,” kasema, “siku moja Roho Mtakatifu atakuja” kufanya jambo lile lile Yeye alilokuwa akifanya. Kasema, “Neno moja dhidi ya Huyo halitasamehewa.”

¹⁸¹ Vema, walifanya nini kwenye Siku ya Pentekoste walipowaona watu hao wakipiga mayowe, na kucheza, na kutenda kama walevi, na kupiga mayowe, na kupiga makelele, na kuendelea? Walisema nini? Walisema, “Wamelewa divai, wao ni walevi,” na yote namna hiyo, Matendo 2. Nao wakawafanyia mzaha na kuwaita kila kitu. Nini kilitukia? Iliwatia muhuri nje ya Ufalme wa Mungu. Mnaona?

¹⁸² Ndipo basi wakati kule kuzingirwa kwa Yerusalemu kulipokuja, sasa, tutalipata hilo katika Ufunuo 7, tutarudi moja kwa moja kwake, yeyote aliyeuliza swali hilo, tutarudi moja kwa moja kwake, na halafu, na wakati wao, Tito akiziteka hizo kuta, historia inasema, juu ya—juu ya Josephus, yule mwanahistoria wa mwanzoni aliyetembea katika siku za Bwana wetu Yesu, naye alikuwa ni mwanahistoria mashuhuri, alisema ya kwamba hata damu ilitiririka, ilibubujika tu kutoka malangoni namna hiyo, waliwaua wengi sana wa hao mle ndani kwa wakati mmoja wakati walipoingia.

¹⁸³ Sasa, Biblia inabashiri ya kwamba katika siku za mwisho kwamba Yeye ataunasa Ukatoliki, Urumi, na mambo hayo yote, na hao wengine, ukomunisti, na wote, pamoja katika mabonde ya Megido kule, mpaka kutakuwako na mauaji makubwa sana kati yao, hata damu itatiririka kwenye lijamu ya farasi... hatamu ya farasi. Mnaona, hiyo ni katika Ufunu-...hiyo itakuwa katika...

¹⁸⁴ Lakini ashukuriwe Baba wa Mbinguni, Sidhani tutakuwa hapa, kwa neema Yake, hatutakuwa, tutakuwa Utukufuni wakati huo, mnaona. Hiyo itakuwa mara baada ya wale ma—ma—manabii wawili kutabiri katika vita vya Har-Magedoni. Hapo ni wakati hizi—wakati nchi hizi za Mataifa zitakapokuwa ovu sana, zinaendelea tu, na muungano wa makanisa, na haya yote yaje pamoja, Naye Mungu atalichukua Kanisa, Kanisa Teule alipeleke Nyumbani kutoka kwa kila moja. Na wanawali wote waliolala watakuwa wakingoje-...

¹⁸⁵ Sasa, lijamu ya hatamu hapo itatoka kwa wale wanawali waliolala na hao wote huko nyuma katika siku hiyo, na ukomunisti, wakati wote wamekutana kule, naye Mungu alisema angewasihii kama alivyofanya katika—katika siku zilizopita, mwajua, kule kwenye bonde hilo. Na hapo ndipo itakapopanda hata kwenye lijamu za hatamu za farasi.

¹⁸⁶ Mlilipata neno lile? Je, wao...? Loo, wangali wanaangalia-...Loo, ni, endeleeni, ni sawa.

[Zile roho tatu chafu ni akina nani?]

¹⁸⁷ Zinazotoka katika, Ufunuo, zinatoka katika kinywa cha yule nabii wa uongo, na yule joka, na kadhalika.

¹⁸⁸ Sasa, tutalipata hilo katika somo letu sasa, mnaona, hizo roho tatu chafu ni *itikadi* tatu. Hebu niwape mfano sasa na mtaona ma—mahali zilipoanzia, mahali zilipoanzia. Mnaona, kulikuwako na ukomunisti, ufashisti, Unazi, zilikuwa ni roho. Ukomunisti ni roho, inakuingia. Unaona? Ni roho. Na hizo, zitakuwa ni kitu kama hicho, ila tu ningeninii...ni—ni... Hilo kweli silo, bali zitakuwa ni roho tatu, namna hiyo tu, ambazo kwa namna fulani zilikuwa mtangulizi wake. Lakini, bila shaka, mnajua ni wapi, ni katika Ukatoliki, mnaona, lakini ningeninii...Ni—ninataka kupata mambo machache juu ya hilo

moja kwa moja kabla ya kulisema, mnaona, nipate kuwa na hakika kwamba ninajua yale . . .

¹⁸⁹ Lakini ni roho tatu, kama tu ukomunisti, ufashisti. Nasi tulitoa hilo miaka mingi iliyopita, mwajua. Mnakumbuka, niliwaambia, nilisema itakuwa ni—itakuwa ni ja—jambo fulani lingetukia, lingekuwa, yote yangeishia katika ukomunisti? Na hapo ndipo inapofanyika, hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati huo, mnaona, itakuwa ni zile roho tatu za uchafu zitakazoenda. Ni . . .

¹⁹⁰ Kweli, kwa kweli ninaamini sasa hivi, ili kulielezea tu kwa urahisi, kama hamjali, na kama mimi—kama nikiongeza zaidi kidogo kwake nikianza kulielezea, vema, mnasema, “Hukulielezea hilo kabisa kule chini usiku ule.” Mnaona? Nikifanya hivyo.

¹⁹¹ Hivi ndivyo ninavyofikiri ingekuwa: Ninaamini ni roho, bikira aliyelala, muungano wa kanisa; Dini ya Kiyahudi juu ya kumkataa Kristo, Wayahudi walioikataa; na Ukatoliki. Kwa sababu, mnaona, mahali ilipotoka, ilitoka kwa nabii wa uongo, mnaona, kutoka katika kinywa cha nabii wa uongo ambaye alikuwa ni upapa, kutoka kwa yule mnyama, mnaona. Na hayo yote, mahali ilipotoka, mnaweza kuona hiyo misingi, mahali ilipo.

¹⁹² Nazo hizo ni zile roho tatu chafu zinazouweka ulimwengu mzima kwenye Har-Magedoni, mnaona. Na hizo ni zile roho tatu chafu; ndipo mnalipata hilo moja kwa moja pamoja na zile ole tatu. Mnakumbuka hivi majuzi, ndiyo kwanza niliingize ndani, nilisema, itakuwa ni yale mapigo saba ya mwisho, mihuri saba, na ole tatu, na ninii mbili . . . roho tatu chafu, na hizo—hizo zinakuja kupitia hapo.

¹⁹³ Sawa, una lingine, sivyo?

[Linasema, “**Mto Frati una umuhimu gani katika Biblia, tukinena kiroho?**”]

¹⁹⁴ Naam, Mto Frati, daima umekuwa ni mto mashuhuri, kwa sababu Mto Frati una nafasi kubwa katika Biblia. Kwanza kabisa tunaona, ya kwamba ulitiririka moja kwa moja kupitia Edeni, Mto Frati ulipitia, Biblia inasema unapitia moja kwa moja Edeni. Jambo la pili tunaona, Mto Frati pia ulikuwa ni mto ulioshuka moja kwa moja kupitia Babeli, mto ule ule, mnaona, Mto Frati ulipitia moja kwa moja Babeli.

¹⁹⁵ Sasa, tunaona ya kwamba yule Malaika alimimina bakuli lake juu ya Mto Frati na kuukausha, kusudi Mfalme wa Kaskazini aweze kushuka. Nami nafikiri hilo kweli litakuwa, litakuwa katika wakati wa mwisho watakapoingia Har-Magedoni, mnaona, inawabidi kushuka moja kwa moja kupitia Misri kule, kuingia mle, na moja kwa moja kupitia nchi hizo, itawabidi kuvuka Frati wapate kuingia mle.

¹⁹⁶ Mnaona, Mto Frati unatiririka siku hizi, tu—tunajua hilo, mnaona, na—na Amazoni, Marekani Kusini, na—na Nile katika Misri, na Frati, na . . . Loo, huo mwingine ni upi? Kuna mito miwili mle ndani, iliyoelekea kule mwanzoni mwa Edeni. Na M—Mto Frati ni wakati hii ninii kuu. . . ilipofanya njia upate kushuka, mnaona, akimfanyia njia Mfalme wa Kaskazini apate kushuka, wale wafalme. Hilo litakuwa, hilo litatukia katika wakati wa vita vya Har-Magedoni katika siku za mwisho, mnaona, ule Mto Frati.

¹⁹⁷ Je, ni hayo tu? Au hivi . . . ? Hakukuwa na lingine.

¹⁹⁸ Sasa, niani mwangu tu, mnaona, kuhusu hilo, jinsi mtu huyu alivyo kama wakimkataa Kristo. Ni ninii tu, huenda ukajitafutia mwenyewe kwenye—kwenye, kwenye kamusi, kwa sababu si jambo ambalo ningeninii, nisingelitaja, papa hapa sasa. Lakini lichunguze, nawe utaona maana yake. Ni . . . Ungeweza tu, kwa maneno mengine, kuna sehemu mbili ama tatu katika Maandiko ningeweza kuwaelekeza, mambo kama hayo.

¹⁹⁹ Kama vile, kwa maneno mengine, kama vile Mfalme Nebkadreza alivyosema, “Mtu yeyote ambaye hange—ambaye hangesujudia huyu *Nanii*,” chini ya, Mungu wa Danieli, na kadhalika, “nyumba yake na iondolewe, watoto wake wachomwe moto, nyumba yake ifanywe lundo la samadi.” Mnaona? Nasi tunatambua maneno hayo ni nini, yanatolewa tu na kusemwa namna hiyo. Lakini ukiangalia tu nyuma katika kamusi, ita—itakwambia tu kwamba ni nini, unaona, kwamba hiyo ni nini.

²⁰⁰ Vema, maskini mambo haya madogo yanaelimisha, nami si—si—sikuweka mengi kwayo kama hayo . . . kadiri ningalipaswa kusimama na kuweka, kwa sababu mnaona, ni—ni ninii . . . kila mtu, ninyi nyote mnaifanya kazi kesho, nami ninaenda, Bwana akipenda, huko Miami. Na ni saa nne na robo, nami sitaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi, nami nafikiri watoto wangu wamelala, na ninadhani na wenu pia, na kwa hiyo haya basi. Na—nao hao jamaa wadogo wanashikwa na usingizi upesi.

²⁰¹ Lakini ninataka kusema ya kwamba hayo ni maswali mazuri, mazuri, sana, kila moja la hayo, mazuri sana. Nami natamani kwamba, kama nina usiku mwingine wa maswali, ama *kitu kama hicho*, maskanini, kwamba ninyi nyote, kama nikilitaja asubuhi hiyo, mngenipa hayo maswali ili ni—nipate muda kidogo wa kuyasoma.

²⁰² Kama mjuavyo, ni harakaharaka tu, halafu u—unaanza kuzungumza, nami ni mtu hodari kwa kuchukua wakati mwingi sana juu ya chochote. Na hapa, mnaona mbinu yangu katika kuhubiri, hiyo ndiyo sababu ninakaa hapo karibu siku nzima, mnaona, ninahubiri tu muda mrefu kupita kiasi.

²⁰³ Lakini mlimwona Billy Graham? Sasa, Billy Graham ni mhubiri aliyefunzwa, naye ni mtu mashuhuri. Naye Billy

Graham, ataweka somo lake papo *hapa*, yeye atarudi nyuma *hapa* nje na kuendelea tu kulishindilia somo hilo, anaendelea tu wakati wote. Ni vigumu yeye kuiacha sauti yake ishuke, anaendelea tu kulishindilia somo hilo. Mnaona? Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu anavyomfanya ahubiri, mnaona, hiyo ndiyo mbinu yake ya kufanya hivyo, hivyo ndivyo anavyolifanya.

²⁰⁴ Charles Fuller, wengi wenu mmemsikia, yeye ni mzee mzuri sana. Na kwa hiyo, Charlie Fuller ni kama mfafanuzi wa Biblia, yeye ni, yeye anapenda ku—kufundisha na kuninii, jinsi anavyoenda mambo, mwajua, na kila kitu, anayaweka tu katika Kristo, na ni mwalimu mzee mashuhuri. Mnaona yale anayofanya, yeye hahubiri, anafundisha tu.

²⁰⁵ Vema sasa, kama mkiangalia, ile njia ndogo rahisi niliyo nayo, ninaweka somo *hapa* nje, hata somo langu liwe ni lipi, Ninarudi *hapa* nyuma kabisa na kuchukua muktadha wangu, na kuuleta *hapa* na kuuweka moja kwa moja sawasawa na somo langu, kisha narudi *hapa* na kuchukua kitu kingine na kukileta *hapa* na kukiweka *hapa* chini, kisha ninarudi *hapa* na kuchukua kitu kingine, mpaka nitakapoyaleta yote *hapa* chini vyema, ndipo basi nayaleta yote kwenye hilo somo, yote tu kwa wakati mmoja.

²⁰⁶ Ndiyo sababu nilikuwa na mahubiri haya madogo niliyokuwa nikijaribu kuhubiri, bila shaka, mmekuwa karibu nami kwa muda mrefu na mnajua mimi si mhubiri, lakini kama vile, *Je, Unasadiki Haya, Nena Na Huo Mwamba, Njoni Mmwone Mwanamke*, na yote namna hiyo, mwajua, maneno madogo matatu tu. Ninii tu, ningeyajenga yote karibu na yule mwanamke kisimani na jinsi ilivyokuwa, kisha mwishoni niushindilie moja kwa moja, ndipo muone, “Njoni Mwone Mtu! Njoni Mwone Mtu!” na “Nena Na Huo Mwamba!” Ninawachukua Israeli na kuwatoa, na mnaona, ninachukua muktadha wangu, na kuuweka hapa kulingana na somo langu, kamwe sijalifikia somo langu bado.

²⁰⁷ Nanyi mliona muda mfupi uliopita katika kuelezea jambo hilo, muda mfupi tu uliopita, jambo lile lile, juu ya yule Mrumi pale, mnaona, akisema, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka.” Mnaona, hilo ndilo swali, kuokoka. Mnaona, nilirudi nyuma, na kuona hayo yote yalikuwa nini, na kuyatoa, kisha nikarudi, kisha nikamchukua Ayubu, na hao wote, nikalivuta hapa barabarani, na kisha nikaliendesha chini, “Hivyo ndivyo ilivyo, ni imani, mnaona, Ayubu alitumia imani, yule Mrumi alitumia imani, tumeagizwa kutumia imani katika kila kitu.”

²⁰⁸ Mnaona, ninii tu, nami ninawazia hivyo kama mimi, katika kulifanya kwa njia yangu, kama ninaweza kuwafanya watu wavutiwe vya kutosha kusikiliza kile unachotaribu kujenga, ndipo unahifadhi somo lako kuu hapa liwe ndilo jambo muhimu la mwisho, kisha uliingize ndani. Ndipo msemi, “Loo, hayo

mengine yanafunguka,” maana, mnaona, mnaliona. Mnaona, ulininii tu, ulinyosha mkono hapa, na kupata mstari uliolekea, ukaingiza hili ndani; basi—basi shida yake ni kwamba, ninaacha mistari mingi sana iliyolekea, kwa hiyo mimi, ambayo—ambayo siipati.

²⁰⁹ Vema, kweli imekuwa ni vema sana kwenu nyote, kuja huku chini, na kuketi na kuzungumza nasi, na kila kitu, nami ninathamini hilo. Nami nataka kusema tena, kwa moyo wangu wote, ninamaanisha hili kwa yote yaliyo ndani yangu: Kamwe sikutambua ni gharama kubwa jinsi gani ninyi watu mnalipa. Ni—nilininii tu, kama isingalikuwa ni kwa ajili ya kuwaona, na haikuwa kwa sababu ya kuwapenda, na mambo ninayofanya, ningesema, “Sitahubiri, maskani hiyo wakati mwingine,” kuona inawabidi ninyi nyote kuendesha maili elfu moja mia nane kwa safari moja kwenda na kusikiliza ibada.

²¹⁰ Sasa, ninathamini huo uaminifu mkuu, lakini hata hivyo, ninawazia yale mnayofanya. Mnaona? Hmm! Nami na—namtumainia tu Mungu ya kwamba kila mmoja wenu katika ile Nchi ng’ambo ya mto, ninyi pamoja na watoto wenu, watoto wenu wachanga na kadhalika, kwamba nita—nitawaona huko ng’ambo, nami natumaini nitakuwako, mimi, nikitumaini nitakuwako.

²¹¹ Nitamwona kila mmoja wenu, na—naomba hata mmoja wa watoto wenu asipotee, hata mmoja wenu asipotee, sisi sote na tuwe kule kwenye Siku hiyo, na—na hata kwa maskini dada yetu huko nje, maskini—maskini mama mweusi huko nje, akiosha vyombo, huko nje katika—katika chumba kingine. Ni—ninakumbuka hapa chini siku moja, nikizungumza na mwanamke huyo, ninaamini (Je, huyo ni mwanamke yule yule?), na mumewe, niliamini ni—nilikutana naye kule wakati mmoja, ama sivyo, ni mvulana anayekufanyia kazi, alionekana ni maskini jamaa mdogo mzuri. Na—natumaini tu sote tutakutana kule ambapo sisi, hakutakuwako na masikitiko, hakuna kuketi tena usiku sana, kwa sababu hakutakuwako na usiku.

²¹² Loo, ndugu yangu, dada, laiti ningaliweza—laiti ningaliweza kuelezea kwa njia yoyote jinsi ilivyokuwa asubuhi hiyo, nilipokuwa nimelala pale karibu na maskini mke wangu pale, na—naye akaninua kutoka kwenye kitanda kile na kunipandisha kule juu, na kuniruhusu niangalie ng’ambo ya pazia.

²¹³ Laiti ningalikuwa na nguvu sasa kuwaelezea jinsi hilo lilivyoonekana na jinsi lilivyokuwa! Niliwaona wote kule, na wote walikuwa vijana, wala si—singeweza kuwatambua. Mnaona, wote walikuwa wakinijia, na kunikumbatia, na kila kitu, nao walikuwa—walikuwa ni wanadamu. Mnaona? Hakukuweco na manyoya ya namna yoyote, kama vile,

wanavyosema Malaika, sidhani Malaika ana manyoya, ingawa wao wananinii tu—wanasema tu hivyo, mnaona.

214 Lakini Malaika ni mjumbe; ambapo hilo neno linamaanisha “mjumbe.” Kwa hiyo, sidhani wana manyoya na vitu kama hivyo. Lakini ni kwamba tu, wote walikuwa huko, na wote walikuwa na furaha, nao hawakuwa, wasingeweza kuwa vinginevyo ila wenye furaha. Na kama hakukuwako na zaidi ya hayo, ningeninii . . . ingetulipa sisi kwa ajili ya shughuli zote na mambo tunayofanya, na—na yote namna hiyo.

215 Lakini ninawatakeni mninii . . . Ninataka kusema jambo hili, kwamba ninaamini, pia, kwamba Biblia ilisema katika siku za mwisho njaa itakuja nchini, na njaa hiyo haitakuwa ya chakula wala maji, bali ya kusikia Neno la kweli la Mungu. Nao watu wangekimbia kutoka mashariki, kutoka magharibi, kutoka kaskazini na kusini, wakitafuta kusikia Neno la Mungu, nasi karibu tunaishi katika siku hiyo sasa. Mnaona? Wakati . . .

216 Sio kumdharau mtu yeyote, mnaona, sio kuyadharau makanisa yetu, la, bwana, lakini kama mnajua, ninaamini ya kwamba katika mimbara ya mengi ya makanisa haya, tuna wanaume wazuri, watu wazuri, watu halisi wa Mungu, lakini wanaogopa kama wakisema jambo lolote ambalo ni kinyume na yale madhehebu hayo yasemayo basi watafukuzwa, kisha wanaachwa kwenye baridi.

217 Nami ninaamini anachohitaji huyo mtu ni ujasiri kidogo. Nami ninaamini ya kwamba, mbona, ninaamini Mungu anataka kumchukua mtu fulani na kutoa mfano kuonyesha ya kwamba Yeye atawashughulikia, bila kujali madhehebu yao. Kwa hiyo, hivyo ndivyo nilivyo, natumaini atafanya nami, kunisaidia, kuniruhusu . . .

218 Na kama mimi, basi sikilizeni, Wakristo, iwapo kamwe wakati mmoja, ni—nita . . . Ninawaagiza mbele za Mungu na—na Malaika wateule, ya kwamba mfanye hivyo, kama wakati wowote mkiona kwamba ninafanya jambo baya, si mje mniambie tafadhali? Maana na—na—nawapenda sana sitaki kuwakosa huko, nami ninajua mnaenda, kwa hiyo mimi . . . njoo uniambie, kama ukionia niko makosani wakati wowote, jambo ninalofanya ambalo si sahihi, kitu ambacho kingeweka jiwe la kujikwaa njiani mwako.

219 Sasa, kuna mara nyingi, mimi huja hapa na kucheka, na kukatakata, na kusema mambo. Ninajaribu kufanya nini? Ninajaribu kuachilia baadhi ya hizo hisia za uchungu zilizoko ndani yangu, mnaona. Ninii tu, si kwamba ninataka kufanya hivyo, mnaona, si kwamba ninataka hata kucheka, ama na kushuka kuja hapa na kukutana na Ndugu Welch ili niweze kumsikia akisimulia jambo fulani dogo kuhusu, loo, yule—yule mvulana mdogo, mvulana mweusi huko nje, basi alimkamata samaki, naye mlinzi wa gereza akamshika, na kusema alikuwa

akishika vyambo vya kasa, na—na kama, kitu fulani, mwajua, kama hicho.

220 Na maskini yule, wakati maskini yule mhubiri aliponiambia. . . Nilikuwa nikiwaambia, hao wasichana wadogo leo hii, kuhusu maskini yule mbwa pudo mdogo kwamba ni Fefe na Fifi, mnaona. Na—na kama, kwa nini ninafanya hivyo? Ku—kucheka, kujiangulia kicheko, ku—kujishusha chini.

221 Unapopanda juu ya milki hii ipatikanayo na mauti ukaingia katika milki hizo *kule*, ni, inakufanya ushikwe na msukosuko, unajua ninalomaanisha. Na halafu hebu wazia tu, hili hapa, wazia tu, pamoja na huduma hii, mnakumbuka yale yatakayonipasa kuwajibikia? Si tu kwa ajili ya Tifton, Georgia, si kwa ajili ya Indiana, si kwa ajili ya Marekani, bali sina budi kuwajibika mbele ya ulimwengu, kwa ajili ya huduma ya ulimwenguni kote. Mnaona? Sina budi kuwajibikia makafiri, sina budi kuwajibika kwa Mungu kwa ajili ya makafiri, hasa, mnaona.

222 Basi ninapoketi nyumbani na kuwazia, “Vema, naamini—naamini—naamini. . .” Kama vile hivi majuzi kule juu, nami nilivurugika moyo sana, ndipo nikasema, “Ni—ni—ninaendelea, nifanye mkutano mwingine.” Nami ninaendelea, ninafanya mkutano mwingine, na muda si muda mwajua, nina uchungu sana moyoni, si—sina budi kwenda kuwinda, sina budi kwenda kuvua samaki, sina budi kwenda huko nje na mtu fulani, si—sina budi kufanya jambo fulani, maana mimi ni mwanadamu tu, mwanadamu tu, mnaona, na hilo—hilo ndilo, mnaelewa hilo.

223 Lakini kama ukiwahi kuwazia ninakosea mahali popote, wewe njoo uniambie, nitalikomesha, jamani, kama tafrija ya. . . haidhuru nini kitatokea. Maana na—nawatakeni mwelewe, sina siri, kila kitu nijuacho, mnajua pia, mnaona. Yote ambayo Bwana amenionyesha, ambayo ataniruhusu kuyasimulia, nimeyasimulia, wala sifichi chochote. Na—nayo maisha yangu yako wazi, mnajua kile nilicho na kile nilichoumbwa kwacho, nami ninaninii tu, ninajaribu kuishi kila siku kadiri niwezavyo.

224 Bila shaka, mara nyingi mnaniona ninapokuwa nimenuna, nami ninajisikia vibaya, na mchovu, na nimedhoofika, ama kitu kama hicho, bila shaka, mimi, hilo linaambatana na huduma, mwajua, mnatambua hilo. Ukininii, kama ukiangalia nyuma kupitia kurasa za wakati, utaona ya kwamba watu ni hivyo, walifanya hivyo, sote tunawaona hao. Lakini jambo ni kwamba, tunataka kuelewana sisi kwa sisi.

225 Ninatambua ya kwamba ninyi mna mema na mabaya yenu pia, si mimi tu niliye nayo, mnayo. Nawe unapokuwa na yako, nitajaribu kuelewa; wakati ninapokuwa na yangu, wewe jaribu kuelewa. Na ninapokuwa ng’ambo mahali fulani, ama huko mbali sana mkutanoni mahali fulani, nao pepo wako kila mahali, wakilundikana na kunipa changamoto na kadhalika, mbona,

nyote kumbukeni, niombeeni tu. Mtafanya hivyo? Tunaweza kuwa na neno dogo Kwake sasa?

226 Baba wa Mbinguni, limekuwa ni jambo tukufu kusimama hapa na kuzungunza na kundi hili la watoto waliooshwa kwa Damu. Ninatambua, usiku wa leo, ninasimama kama tu vile Mtakatifu Paulo alivyosimama miaka mingi iliyopita, mikutano midogo ya nyumbani mahali walipokutanika. Ndipo Paulo akaja kwa Akila na Prisila, na—na jinsi ambavyo hapana shaka walikuwa wameninii, wamewakusanya watu mle ndani. Naye akaenda, Rumi na akapangisha nyumba, naye akawapokea wale walioingia.

227 Na hapa usiku wa leo, watu kutoka, wanaokuja maskanini, na—na watu ambao, wanaendesha maili hizi zote, ambao nimekuwa tu nikijaribu kuwaambia jinsi ninavyoathamini jambo hilo. Bwana, hata sina maneno, ninayoweza kuwaambia kwayo, jinsi ninavyowathamini, lakini Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utawafanya wajue mioyoni mwao kile ninachomaanisha.

228 Na, Mungu mpendwa, kama... tafadhali, ninaomba ya kwamba utajibu maombi yangu kwa ajili yao. Waokoe kila mmoja wao, Bwana, jalia kusiwe hata mmoja wao atakayepotea, ama yeyote wa familia zao apotee, jalia wao, kila mmoja, awepo.

229 Ninawaombea watoto wao. Namwazia mvulana huyu mdogo aliyelala hapa pajani mwa baba yake, na mama yake ameketi, akiangalia, na kuwazia juu ya siku zijazo. Kama kuna kesho, ninajuaje ya kwamba mvulana yuyo huyu mdogo hatahubiri Injili? Mungu, ninaomba ya kwamba utambariki huyu mvulana mdogo, wengine wote, wasichana wadogo na wavulana, na uwe pamoja nao wote. Kuwa pamoja na Ndugu na Dada Evans ambao wamefungua nyumba yao, nyumba ya maombi. Kuwa pamoja nasi sasa na utusamehe dhambi zetu.

230 Na Mungu, kama wakiwahi kuwa wagonjwa na iwabidi kupiga simu, Mungu, jalia niishi maisha ambayo wataamini ya kwamba Wewe utanisikia, kisha unisikie ninapowaombea, Bwana, lijalie. Nawe usikie, wakati wanaponiombea, maana ninahitaji maombi yao, Baba. Na kila wakati wanaponiombea, hivi hutasikia, Bwana? Ninapowaombea, sikia, Bwana.

231 Nasi pamoja tutakutumikia Wewe maishani mwetu mwote. Na katika ile Siku kuu, tunatumaini kuja Nyumbani Mwako siku moja. Na wakati tutakapobisha mlangoni, hivi hutaturuhusu kuingia, Baba? Hadi wakati huo, utulinde, na utubariki, na utudumishe waaminifu daima, tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

232 Asanteni sana, jamani. Nami ninasikitika kuwaweka hapa mpaka—mpaka karibu saa nne na nusu. Maskini mvulana huyu aliyelala hapa, amelala kama askari mdogo. Ana umri gani?...?...

233 U hali gani, Dada, sijui kama nilikupa mkono nilipoingia au la. Vema, ni vizuri kukuona tena, na wewe, Ndugu Willie.

Fred, nadhani utaondoka asubuhi, ukirudi kuelekea nyumbani. Unarudi na mamba wa—wangu?

Tuonane nyumbani, Ndugu Wood, Bwana akubariki.

234 Wewe, Ndugu Scott, nimefurahi kukuona tena, Ndugu. Ninaamini nimekuona hapo awali mahali fulani, sivyo? Nilidhani nimekuona, uso wako unajulikana.

235 Ndugu Wayne, Bwana akubariki. Na bado nafikiri yanipasa kujaza tangi lako kwa petroli kwa ajili ya kuja huku maili themanini kumleta mhudumu huyu, pia. Ubarikiwe, Mwanangu.

Ubarikiwe, Dada. Na kukutania kwangu kote, ninakutania tu. Unajua hilo sivyo?

236 Mungu akubariki, Dada Evans. Hicho kilikuwa kizuri kweli, kiamshakinywa, na chakula cha jioni, na ukarimu wenu mzuri, kumbukeni, Yesu alisema hivi: “Kadiri mlivyomtendea aliye mdogo sana . . .” Sasa, Yeye kamwe hakusema, “Kadiri mlivyomtendea aliye mkuu sana . . .” Mnaona? Mnaona, huyo huenda, huyo angekuwa ni mtu mwingine, lakini “Kadiri mlivyomtendea aliye mdogo sana . . .” mnaona, hiyo ingekuwa ni mimi, kwa hiyo umenitendea mimi.

237 Nimefurahi kukuona tena pia, Dada. Mungu awe pamoja nawe daima. [Dada huyo anasema, “Huyo ni mama yangu. Nadhani unamkumbuka.”—Mh.] Mimi . . . Loo, jamani. Ungewezaje kusema haikuwa ni mama yako? Mnafanana sana.

238 Ninafurahi kukuona, Dada. Ninaamini wewe ni mke wa, jamaa huyu kijana *hapo*. Nawe ni Ndugu Scott. Ninyi nyote ni dada? Vema, nilidhani ninyi ni dada, hakika nilifikiria hivyo. Ni vema kukuona tena. Na uendeleo kuwa na moyo wa ushujaa, ndugu yangu.

Na aisee, labda huyu ni mpya, sikumwona msichana huyu hapa. Loo, vema, nina furaha kukutana nawe, Dada. Bwana akubariki.

Ni vema kukuona, Dada. Naye atakuwa mwema kwa kitu fulani, mchukue tu. Mungu akubariki, Ndugu.

Ndugu Evans, Mungu awe pamoja nawe, Kijana.

Sasa, Mpenzi, naomba uwachukue watoto wetu, afadhali tuondoke.

Mungu akubariki, ndugu yangu.

239 Na, nawaambia, kabla hatujaondoka, hebu na tusimame tu kwa miguu yetu na kuimba wimbo huo mdogo. Je, mtaimba kifungu kidogo pamoja nami, namna hiyo? Ni sawa?

Mungu awe nanyi hata tutakapokutana tena!

Kwa maonyo Yake awaongoze, awashikilie,

Pamoja na kondoo Wake awafungie salama;
Mungu awe nanyi hata tutakapokutana tena!

Hata tutakapokutana! hata tutakapokutana!
Hata tutakapokutana miguuni pa Yesu;
Hata tutakapokutana! hata tutakapokutana!
Mungu awe nanyi hata tutakapokutana tena!

²⁴⁰ Hivi ndivyo tulivyokuwa tukifanya kwenye mikutano midogo ya maombi, hebu na tushikane mikono, moja kwa moja kuzunguka namna hii, mnaona. Tunaimba wimbo huu mdogo, tufanye duara ndogo, tuwe pamoja, hivyo ndivyo, mnaona. Mnashikana tu ninyi kwa ninyi namna hiyo, sasa. Hebu tuimbe. Je, mnaujua wimbo huu mdogo?

Kibarikiwe kifungo kiifungayo
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama ule wa huko juu.

Mbele ya Kiti cha Enzi cha Baba yetu,
Tunamwaga maombi yetu pamoja;
Hofu zetu, matumaini yetu, malengo yetu ni
mamoja,
Faraja zetu na mahangaiko yetu.

Tunapoachana,
Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutaungana moyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

²⁴¹ Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu na turudie tu ombi hilo la mfano:

Baba yetu, uliye Mbinguni, Jina Lako
Litukuzwe.

Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike
duniani, kama huko Mbinguni.

Utupe leo riziki yetu ya kila siku.

Na utusamehe makosa yetu, kama nasi
tuwasamehevyo wale wanaotukosea.

Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule
mwovu; kwa kuwa Ufalme ni Wako, na
nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

²⁴² Mungu awabariki, kila mmoja, sasa, hata tutakapokutana tena.

Ndugu Welch, unamaanisha una hayo yote kwenye kanda kule chini? Hmm!

²⁴³ Vema, laiti ninyi nyote, mngalikuja mwende Florida pamoja nasi. Bwana akipenda, na—nawaambia ninalofanya, ninajaribu kuwatoa watoto, mnaona, wao ni, hawakuweza kumaliza likizo yao, nyanya yao alikuwa na mshtuko wa moyo ikatubidi kurudi. Kwa hiyo basi ninawatoa nje kwa namna fulani kumalizia likizo

yao, maana hawana budi kuanza shule tena, mara moja. Kwa hiyo nitawapeleka mahali fulani kesho, labda huko chini St. Petersburg, ama mahali fulani.

²⁴⁴ Sina budi kurudi, labda, kabla ya Jumapili. [Ndugu Evans anasema, “Wana baadhi ya hiyo mifugo kule chini, nafikiri, unajua, kwenye jumba la makumbusho, unajua, ulilokuwa ukizungumzia muda mfupi uliopita.”—Mh.] Loo? Naam? Vema, ningependa kwenda huko niwaone. Hiyo ni kweli. Sijawa kwenye jumba la makumbusho kule chini. Hiyo ni, ilikuwa ni wapi? Jumba la makumbusho la Ripley. Na hiyo ni huko St. Petersburg? Huko chini Saint, ninamaanisha huko St. Augustine, badala yake.

²⁴⁵ Naam, ninaenda hapa kwenye, hii ni Jacksonville ndiko ninakoenda kwanza, sivyo? Naam, huko nyuma, maana ninakigeuza kitu hiki, kurudi *huku* Jacksonville, halafu ninapitia La Crosse, mnasema, na huko nje kupitia huko? Waycross. Uh-huh.

²⁴⁶ [Ndugu mmoja anasema, “Ninaanza kuwazia, uliuliza. . . ulitaja kwamba uliigeuza, maskani inaangalia upande gani?”—Mh.] Maskani inaangalia mashariki na magharibi. Niliijenga. . . Unapokuja kutoka u—upande wa mbele, unajua mahali Barabara ya Nane inapoelekea *huku*, unaelekea moja kwa moja mashariki basi. Unaona? Halafu basi, ile—ile. . . Halafu ukisimama. . . Na wakati ninapohubiri, ninahubiri kuelekea magharibi, na mnaona, sasa, ninafanya hivyo ili kwamba madhabahu iwe mashariki, kwa sababu Yesu anakuja kutoka mashariki. Ndipo basi hiyo—hiyo huniwezesha. . . Madhabahu, tunasujudu daima kuelekea mashariki, mnaona.

²⁴⁷ Vema kwa kawaida, sijui, ni yale tu niliyofanya daima, ninaona katika Biblia, wao, kwa kawaida huko nyuma, Danieli alisema alienda na kuyafungua madirisha, mwajua, na kadhalika namna hiyo, na kuomba, akielekea mashariki.

²⁴⁸ Na—na kwa hiyo, nami niliona katika lile hekalu la kale la Musa, nafikiri, lilielekea mashariki, madhabahu ilikuwa hivyo. Na kwa hiyo, bila shaka, Mungu atakusikia popote ulipo, unaona, haidhuru.

²⁴⁹ [Huyo ndugu anasema, “Kamwe nisingeweza kupata mwelekeo sawa.”—Mh.] Naam, bwana. Vema sasa, nimeona wakati ambapo nimeomba sana na kadhalika, Mimi—mimi kamwe sininii—mimi kamwe sigeuki, mnaona, ninakuja tu huku.

²⁵⁰ Lakini sasa, kama siangalii, na kitu chochote kama hicho, halafu nishuke tu chini na kukirukia, nitaninii tu. . . Kuna pawili. . . mahali pamoja ninapopajua, ambapo kamwe siwezi kupafahamu vizuri, na hata hivyo ninajua palipo, na hapo ni huko chini kwa Nyanya Cox. Ninaweza kwenda kule chini, nami siwezi kupafahamu hapo vizuri. Na kutakuwako na kitu

fulani, kinachoonekana kwangu kama, kitatokea kule siku moja. Ninaenda papa hapa kwenye lango hili, nalo, huko ni kuelekea kusini tu iwezavyo kuwa, nikigeukia mkono wangu wa kulia, lakini sivyo, mnaona, sivyo, ni vinginevyo. Mnaona? Nami ni—ninaninii tu . . .

²⁵¹ Na kama nikiingia mwituni, sasa, kama nikipotea ama *kitu kingine*, halafu kama ningeninii, ningegeuka, sasa, kama nikisisimkwa kabisa, vema, si—siwezi kufanya hivyo, mnaona, lakini kama nikisimama tu kimya kwa dakika chache na kusema, “Baba wa Mbinguni, nisaidie.” Na, ndugu, naweza tu kuninii, kukuelekeza huko, kwa urahisi vivyo hivyo, hiyo ni kweli.

²⁵² Wakati mmoja nilitoka, kule pamoja na Ndugu Wood na Dada Wood, tulikuwa tukitoka Chattanooga, naye Ndugu Wood alikuwa akiendesha gari, nadhani hiyo ni 41, akirudi tu. Kwa hiyo, ni—nilikuwa nimechoka sana, loo, nilikuwa nimechoka sana, nami nilijilaza tu nyuma, baada ya ibada, na kujilaza huko nyuma na kulala, nyuma ya gari. Niliamka baada ya kitambo kidogo na kusimama, na nikasema . . . Ukungu? ilikuwa vigumu kuuona mkono wako mbele yako. Nami nikasema, “Aisee, Ndugu Wood, unaelekea kwingine.”

Akasema . . . Mnaona, nilikuwa tu ndio kwanza nitoke kwenye mkutano huo. Naye akasema, akasema, “Loo, la,” kasema, “Ninaenda, mimi,” kasema, “Ninaelekea 41.”

Nikasema, “Lakini una—unaelekea kusini.”

Naye akasema, “Sasa, unawezaje kujua katika ukungu kama huu? Unaona, hata huwezi kuona barabara.”

Nikasema, “Lakini una—una . . . Naweza kujua sasa hivi kwamba unaelekea . . . una—unaelekea kusini.”

Akasema, “La, la. Unaona *pale*, hiyo ni 41.”

Nikasema, “Lakini ni kosa.”

²⁵³ Vema, tukaendesha kidogo, naye akaendelea kubishana nami kwamba alikuwa sahihi, alisema tu, “Niko moja kwa moja kwenye 41, nikienda Memphis.”

Nami nikasema, “Angalia tu.” Ndipo tukaingia kwenye kituo cha petroli, nami nikasema, “Ni umbali gani kwenda Memphis?”

Akasema, “Inakubidi kugeuka, Jamani, uko Georgia.” Kasema, “Rudini upande *huu*.” Kwa hiyo, tungeenda moja kwa moja . . . Naam, bwana.

[Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam, bwana? Naam, bwana. Naam, bwana. Vema, usipoangalia . . .

²⁵⁴ Nami ninakumbuka wakati mmoja, nilikuwa nimepotea huko juu milimani, na hapo ndipo ni—nilipofikiri nilikuwa mtu hodari sana wa mwituni nisingeweza kupotea, lakini kweli

nilipotea. Naye mke wangu alikuwa pamoja nami, naye Billy Paul alikuwa mtoto mchanga.

²⁵⁵ Nao, nikawaacha, na nikaenda—nikaenda kuwinda dubu, mnaona, nami nilikuwa nikiwinda dubu, ndipo—ndipo nikakutana na kulungu dume mkubwa pale. Nilikuwa nimempiga risasi huyu dume, nami nikawazia, “Vema, afadhali nirudi nyuma.” Nami ninajua ningeshuka, nilikuwa huko Adirondacks, basi nikapanda mlima namna *hii*, nami. . . kitu fulani kikavuka barabara, na ilikuwa—ilikuwa ni simba wa mlimani, naye alikuwa amerudisha tu masikio yake nyuma. Naye, kabla tu hajaninii. . . Nikainua bunduki yangu upesi vya kutosha kumpiga risasi, akatoroka, mnaona.

²⁵⁶ Naye Meda hakuwa amewahi kuwa mwituni maishani mwake, mnaona. Na, vema, ilikuwa kwenye wakati huo wa fungate, mnaona. Nami nilifanya kazi nzuri kule, mnaona, wakati ule ule nilipofunga ndoa, ndipo ningeweza, mwajua, nilimpeleka kwenye fungate yetu na kwenda kuwinda wakati uo huo, mnaona.

²⁵⁷ Kwa—kwa—kwa hiyo mimi, nami ni—nikawazia, “Vema sasa, sasa niliendaje?” Mimi, basi nikaja *huku*, nikageuka chini, na kwenda huko, nikagonga mwamba chini ya maji, nikapitia kwenye kifuko kidogo, nilijua nilikuwa huko chini kuelekea Majitu mahali fulani, kuelekea upande wa Canada, lakini sikujua ilikuwa ni wapi hasa.

²⁵⁸ Ndipo ikatokea dhoruba, na mara ghafla, mwajua, hizo dhoruba za theluji. Na, loo, ukungu ulikuwa chini sana, hata usingeweza kuuona mkono wako mbele yako. Na hapo ndipo wewe, katika nchi hizo, afadhali uketi chini kama hujui mahali ulipo, maana utakufa papo hapo, unaona. Basi nenda tu ukajipatie mahali, na kujifungia, na upate kitu cha kula, na kungojea siku moja ama mbili mpaka dhoruba iishe, kisha utoke uone mahali ulipo.

²⁵⁹ Kwa hiyo, nisingeweza kujificha, Meda alikuwa mwituni, na kamwe hajawahi kuwa mwituni hapo awali, katika kibanda-egemezi kidogo, kisicho hata na mlango, ninii tu, mwajua, kilikuwa ni kibanda-egemezi kidogo, namna *hiyo*. Kwa hiyo, mimi huyu katika hali hiyo. Na loo, jamani! Nikaninii, nikaanza kwenda moja kwa moja *hivi*, nikawaza, “Vema, niligeukia *hapa* mahali fulani.” Nikarudi moja kwa moja mahali nilipompigia risasi yule kulungu. Nikaondoka tena, nami nikasema, “Sina budi kutafuta njia ya kutoka hapa, mke wangu na mtoto mchanga watafia mwituni.” Mnaona?

²⁶⁰ Ilikuwa inaingia baridi, na huo—huo ukungu ukipasua, ambapo kutakuwa na theluji katika muda mfupi tu, mnaona. Nami nikaanza kupanda tena, nikarudi kwa yule kulungu tena, nikafanya hivyo mara tatu. Vema, nilijua basi. . . Nikasema, “Vema, ni—ninaenda. . . Ni—niko mahali fulani. . .”

261 Mnaona, sasa Wahindi wanaita hayo “mwendo wa mauti,” uko mahali tambarare, nawe unatembea huku na huku, huku na huku katika duara, unaona. Sasa, ukiwa na dira, hungefanya hivyo, unaona, bali unatembea huku na huku katika duara, Mhindi anakuita, “uko kwenye mwendo wa mauti.” Mnaona? Maana unashikwa na kichaa wakati huo, hapo ndipo wanaporukwa na akili na kuanza kukimbia, wakipiga mayowe, na kadhalika, mpaka hatimaye wanajitosa kwenye genge, ama kitu fulani na kufa, ama labda wanajiua.

262 Halafu basi, na—nakumbuka nilisema, “Vema, ninaenda moja kwa moja. Si—si—sina budi kufika. . .” Ndipo kwa namna fulani nikashikwa na kiwewe, nami nikawazia, “Keti chini. Mbona, ewe maskini mjinga, unajua hujapotea, hu—huwezi kupotea, unaona,” nami nikaendelea kusema hivyo. Vema hiyo, mnaona ha—haikuwapo kamwe. Wakati kuna kitu ambacho hakipo, huwezi kukidanganyia, unajua. Kama tu. . .Na kwa hiyo, nikasema, “Vema, sijapotea, ninajua mahali nilipo hasa, hakika, nilikuja moja kwa moja *hivi*. Hiyo ni kweli kabisa.” Nikiendelea kujizungumzia hivyo, mwajua, huku nikitokwa na jasho sana nilivyoweza.

263 Sasa, kama ningalikuwa peke yangu, ningenda tu mahali fulani, na kuingia mahali padogo, na kungojea mpaka dhoruba iishe, labda siku moja ama mbili, lakini ingekuwa ni sawa, nijipatie kipande cha kulungu wangu na kumwachilia aende, mnaona. Lakini usingeweza kufanya hivyo, huku mke akiwa mwituni, na kamwe hajawahi kuwa mwituni. Mbona, wangekufa usiku huo, hawangejua jinsi ya kujihifadhi mwituni, mnaona.

264 Kwa hiyo, niliwazia. . .Nilikuwa tu nikienda kule ndipo nikasikia Kitu fulani kikisema, “Mimi ni Bwana, Msaada utakaonekana tele wakati wa shida.” Nikaendelea tu kutembea, nikawaza, “Sasa, ninashikwa na kiwewe,” mnaona, “Ninafikiri ninasikia mambo.” Hii ilikuwa tu, tulikuwa ndio kwanza tufunge ndoa, miaka ishirini iliyopita. Nikaendelea tu kwenda *hivi*, Nacho kikasema, “Mimi ni Bwana, Msaada utakaonekana tele wakati wa shida.” Nacho kikasema hivyo mara tatu ama nne.

265 Basi baada ya kitambo kidogo, nikasimama, nami nikawazia ya kwamba “Ama nimerukwa na akili, au Mwenyezi Mungu amenirehemu.”

266 Ndipo nikapiga tu magoti na kuweka bunduki yangu chini, nikasema, “Mungu, nakiri nimepotea,” mnaona, nilisema, “Ni—nimepotea. Na Wewe. . . Kamwe sitaninii. . . Siwezi kamwe kutoka hapa na. . . Nilifikiri nilikuwa bingwa sana wa mwituni nisingeweza kupotea, lakini,” nikasema, “nimegeuka kabisa, hakuna njia,” tayari nimesisimkwa, mnaona, “kwa hiyo hakuna njia kamwe kwangu kupata njia yangu ya kutokea. Na—nami sistahili kuishi, Bwana, lakini mke wangu na mtoto mchanga wanastahili.” Mnaona? “Kwa hiyo, nisaidie kuwafikia,

wasije wakafia mwituni.” Nikasema, “Sistahili kuishi, bali wao wanastahili.” Na—nami nikasema, “Kama utanisaidia tu, nitakushukuru sana.”

²⁶⁷ Nikasimama, nikasema, “Sasa, nitauielekeza uso wangu moja kwa moja *hivi*, nami najua ninaenda moja kwa moja kuelekea mahali nilipomwacha Meda na hao wengine.” Lakini mimi...? . . . nilikuwa nikienda moja kwa moja Canada, mnaona, kwenye mwendo wa mauti, mnaona, nikiingia moja kwa moja Canada.

²⁶⁸ Basi nikaanza namna *hii*, na kwa ghafla, nikahisi Kitu fulani kikifanya [Ndugu Branham anapigapiga kitu fulani—Mh.], mkono, nikawaza, “Ni nani Huyo?” Nami nikaangalia juu, na kwa wakati mzuri tu wa kuangalia nyuma, na ukungu wa kutosha tu umeondoka, mpaka nikaona kilele cha Mlima Hurricane, nao walikuwa wamepiga kambi chini tu ya Mlima Hurricane.

²⁶⁹ Vema, basi nikasimama tu pale na kulia kama mtoto mchanga, nikimsifu Mungu, mwajua, kwa kunisaidia. Ndipo, ilinibidi kutoka kwa njia hiyo, na ikawa giza juu yangu, na—na kulungu na kadhalika wanaruka juu mbele yangu. Lakini sikuwa...Na baada ya giza kuingia...najua mimi na yule mlinzi...kutoka kwenye kibanda hiki cha mlinzi kiko pale pale karibu na kibanda-egemezi, ila kilikuwa kimefungwa. Na halafu, hiyo—hiyo ni maili ishirini na tano kutoka kwenye nyumba iliyo karibu sana na hapo na kuendelea mpaka chini, mnaona. Na halafu hapa juu mlimani, hapa karibu na kibanda cha mlinzi, na halafu kupanda mpaka kwenye ule mnara, huko juu ya kilele kikubwa kule juu, vema, nilijua nilikuwa kwenye kile kilele mahali fulani.

²⁷⁰ Lakini hiyo milima ni maili nyingi, nyingi, nyingi kuzunguka, mwajua, maili thelathini, arobaini, hamsini, kuuzunguka mlima pale. Na kwa hiyo nikawazia, “Sasa, laiti ningaliweza tu kuugusa waya huo unaoshuka chini pale.” Mimi na yeye tuliweka kwa ajili ya simu, mwajua, tukaupigilia kwenye miti, nao unashuka kwenye kituo chake, kisha wanawasiliana kutoka—kutoka kwenye—kutoka kwenye huo mnara, mwajua, mpaka chini kituoni. Halafu alikuwa anakuja katika siku chache kuwinda dubu pamoja nami.

²⁷¹ Ndipo usiku ukaingia, ndipo nisingeweza kuona, mwajua. Basi, ni giza kwa vyovyote vile, kukaingia giza katika yapata dakika thelathini, arobaini, na ilikuwa tu yapata saa nane ama saa tisa alasiri. Lakini ninainua mkono wangu juu namna *hii*, nami ningetembea tu, nami ningeninii tu...ningeishika bunduki yangu kwa mkono *huu* na kutembea, mwajua. Nami nilijua waya huo uko juu karibu *hivi*, ambapo tuliufungia kwenye miti kote kote.

272 Nikawaza, “Laiti ningaliweza kuugusa waya huo!” Nami ningegusa tawi namna *hiyo*, mwajua, nami nikawazia, “*Aha!* La, hilo ni tawi,” mnaona, ningejaribu tena. Ndipo nilipobadilisha, na mkono wangu ungeanza kuuma, nimeuinua kwa muda mrefu sana, ningebadilisha na kuweka bunduki yangu *hapa* na kurudi nyuma hatua kadhaa, mwajua, kuhakikisha ya kwamba sikuuvuka, mnaona, kuwa karibu, na namna *hiyo*.

273 Na, ndugu, kuendelea, na tayari kumeingia giza jeusi kabisa, mwajua, nami nilikuwa nimetembea yapata saa moja katika giza hilo, ndipo mkono wangu ukagusa waya huo, nikauhisi. Vema, niliinamisha tu kichwa changu na kuanza kulia, mwajua, nami nikawazia, “Bwana, moja kwa moja mwishoni mwa waya huu anangojea mke wangu na kila kitu.” Mnaona? Nikawaza, “Hiyo ni kweli.” Nami nikasimama pale na kuinamisha kichwa changu na kumshukuru kwa ajili ya jambo hilo. Nikawazia, “Naam, Bwana, nimeweka mkono wangu katika Wako, ni mkondo, waya, na papo hapo mwishoni mwa waya huu, ambao ninashikilia sasa moyoni mwangu, unashikilia kila kitu ninachopenda,” mnaona, “wapendwa wangu wote, Bwana wangu, Mwokozi Wangu, wote niwapendao wamo mwishoni mwa waya huu.” Kwa hiyo, nisingeuacha mkono wangu uuachilie waya huo, nikaufuata waya huo moja kwa moja chini ya mlima.

274 Ingawa kulikuwako na njia ndogo—ndogo iliyovu... iliyovunjika nusu pale, ambapo tungepandia, mwajua, lakini nisingeiamini hiyo, nilishikilia tu huo waya. Wakati nilipougonga mti, ningejibambua moja kwa moja, nishike mti na kuushika tena, niende mbele kwenye mti mwingine, kisha niushike nikishuka chini, yapata maili tatu chini ya mlima, nami nikafika kule, naye Meda alikuwa karibu ameshikwa na mpagao, mwajua, ninii tu, matatizo chungu nzima. Lakini ndivyo hivyo. Mnaona? Hakuna kitu, hakuna hisia, kama kupotea. Vipi kuhusu kupotea, kupotea mwituni, lakini na kupotea kutoka kwa Mungu je?

275 Vema, Meda? Njoo, Mpenzi, Ndugu Welch hana budi kwenda kazini, na Banks na hao wengine labda watataka kuanza mapema, na hawa ndugu wengine wote wanaotaka kwenda kazini, na dada zetu hawana budi ku—kuwaogesa watoto na... [Ndugu mmoja anasema, “Tuliufurahia vizuri sana.”—Mh.] Asanteni. Asanteni. Kama mliufurahia nusu ya vile nilivyofurahia, kuzungumza nanyi, ulikuwa mzuri sana.

276 Ndugu Welch, asante kwa wakati huo mzuri alasiri ya leo, pia, tuliokuwa nao huko nje pamoja na, kunipeleka huko nje kwenye, hayo mabwawa ya mamba huko nje.

Dada, ninyi nyote, hakika ninawashukuru kwa ajili ya chakula hicho kizuri cha jioni.

[Ndugu fulani anasema, “Asante, kwa kushuka kuja kuwa pamoja nasi, pia.”—Mh.] Loo, jamani!

277 Una msichana mdogo mle ndani, pia? Ana nywele nzuri kuliko zote, niliona alikuwa amesuka, kwa namna fulani nywele za manjano kabisa, zilizoonekana za dhahabu, ambazo—ambazo ni nzuri sana.

278 Ninataka kukupongeza juu ya nywele zako pia, Dada. Najua ni bora zaidi. Ninaamini ulikuwa na nywele fupi, sivyo? Kidogo hadi mabegani mwako, kwa namna fulani imekatwa ama *kwa namna fulani*, ama sivyo? [Dada huyo anajibu—Mh.] Naam. Mimi . . . Naam. Mimi . . . Vema, kweli inaonekana nzuri sasa, unaona.


279 Nilikuwa nikiwaona hawa, wanawake hawa wote hapa, pamoja na nywele zao ndefu na kadhalika, inaonekana kama, loo, ingeweza kuwa nzuri vivyo hivyo kwa njia moja au nyingine, mwajua, kama walikuwa na nywele fupi au la, lakini inaonekana tu *hivyo*, mwajua, mnajua ninalomaanisha. Ninii tu, labda ni mimi tu, lakini . . .

Huyo hapo yule msichana mdogo. Yeye kidogo ana haya, sivyo?

Naweza kumbeba, Mpenzi? [Dada Meda anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Yuko wapi? Loo. La.

280 Unamsikia akiniambia? Ulishika hilo? Alisema ilitubidi kumngojea Becky aje, lakini kasema, “Haimaanishi inakubidi kwenda *kule* na kuanza kuhubiri tena.”

281 Hivi msichana huyo mdogo si ana nywele nzuri pia, kipenzi? Yeye ni biskuti mwenye maskini mtindo wake wa nywele zinazoning’inia chini pale pia, maskini rangi ya stroberi manjano na . . .

282 Mwajua, nitatoka nje nione kama maskini hiyo, niiwashe maskini Kadilaki hiyo ya kale kama nikiweza, Ndugu Welch. Nami nitaninii, samahani kwa dakika moja tu, nami nitaona kama ninaweza, wakati mwingine inakohoa kidogo na kubweka, mwajua, na . . .? . . . 

61-0808 Nyumba Yako
House Meeting
Tifton, Georgia Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org